# JICHO LA HAZINA

Msajili Wa Hazina Zanzibar

www.trosmz.go.tz

TOLEO NAMBA 011 DESEMBA, 2025


MIAKA 62 YA MAPINDUZI

# Sanya: Dkt. Mwinyi chachu ya uimara wa mashirika Z'bar



## TOLEO MAALUM LA MAPINDUZI









# Yaliyomo


03
DKT. MWINYI SHUJAA WA UJENZI WA MASHIRIKA IMARA YA UMMA ZANZIBAR

05
IDARA YA MALI YAZIDI KUWA MSAADA OFISI YA MSAJILI WA HAZINA ZANZIBAR

06
MABORESHO YA OFISI YA MSAJILI WA HAZINA ZANZIBAR

09
MAFANIKIO MIAKA MITANO YA DKT. MWINYI 2020-2025

17
YAJAYO NI NEEMA ZAIDI, UONGOZI UNAOACHA ALAMA VIPAUMBELE MIAKA MITANO IJAYO YA DKT. MWINYI MADARAKANI

23
MAFANIKIO YA MAPINDUZI KWA MAENDELEO YA ZANZIBAR

26
IDARA YA MITAJI YA UMMA YAPATIWA MAFUNZO KUHUSU USIMAMIZI WA TAASISI ZA UWEKEZAJI ZA UMMA

27
WAHASIBU WAKUU WA MASHIRIKA WAFUNDWA NAMNA BORA YA KUANDAA SERA YA GAWIO

28
IDARA YA MITAJI YA UMMA NA UWEKEZAJI YATOWA MAFUNZO KWA BENKI YA WATU WA ZANZIBAR (PBZ) JUU YA KUANDAA RIPOTI ZA UTEKELEZAJI ZA MKATABA WA KIUTENDAJI


**Ofisi ya Msajili wa Hazina inatoa wito kwa kila mdau na mwananchi kutoa mapendekezo, ushauri au lolote lile ambalo anahisi litasaidia kulifanya jarida kufikia lengo lake la kuanzishwa na hatimaye kuchangia katika ukusanyaji, usimamizi na matumizi ya fedha katika taasisi za umma. Kwa kushirikiana na kushauriana ndio tutaweza kufanikiwa kujipatia maendeleo tuliyokusudia na kuwa na Zanzibar tunayoitaka.**




# Dkt. Mwinyi shujaa wa ujenzi wa mashirika imara ya umma Zanzibar

**Na Waheed Muhammed Ibrahim Sanya, MSAJILI WA HAZINA ZANZIBAR**

MAENDELEO makubwa yaliyopo sasa na mikakati iliyopo juu ya uimarishaji wa mashirika ya umma unaofanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi ni mwanzo wa safari mpya wa mashirika kuwa chanzo cha mapato na ukuaji wa uchumi wa nchi.

Hii inatokana na msukumo mkubwa uliopo kutoka serikalini kuja na mawazo bora na yenye kuonyesha mkakati madhubuti unaotoa majawabu ya maswali magumu ambayo awali yalikuwa yanasumbua mashirika ya umma na kuonekana ni mizigo kwa serikali na vichaka vya watumishi kufanya ufisadi.

**MIKAKATI YA SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR KWA MASHIRIKA YA UMMA**

Mikakati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mashirika ya Umma Zanzibar kwa miaka mitatu kutoka mwaka wa fedha 2024/2025 hadi 2026/2027, Serikali imeendelea kutekeleza mageuzi ya kiutawala na kiutendaji yanayolenga kuimarisha usimamizi wa mashirika ya umma.

Malengo ya kufanya hayo ni kuendeleza utoaji wa huduma kwa wananchi, uimarishaji wa uwekezaji wa kibiashara, kukuza ufanisi, uongezekaji wa mapato uwajibikaji, uwazi na matumizi bora ya rasilimali za umma.

Katika kufikia mageuzi hayo, Serikali imepanga mikakati mbali mbali katika maeneo mengi ikiwemo Kuimarisha usimamizi wa Mashirika ya Umma na mali za Serikali.

Ofisi ya Msajili wa Hazina inatarajia kukusanya gawio la jumla ya shilingi bilioni 71 kufikia mwaka wa fedha 2026/2027 kutoka shilingi bilioni 13 mwaka wa fedha 2022/2024, pamoja na kukusanya shilingi bilioni 2 kama uwiano wa mapato yatokanayo na Mashirika ya Umma zisizotengeneza faida, na shilingi bilioni 8.3 kutoka shilingi bilioni 1.4 zinazotokana na mauzo ya mali chakavu na ukodishaji wa bohari na majengo.

**Katika kufikia mageuzi hayo, Serikali imepanga mikakati mbali mbali katika maeneo mengi ikiwemo Kuimarisha usimamizi wa Mashirika ya Umma na mali za Serikali.**

Aidha, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Ofisi imepangiwa kianzio kipya cha ukusanyaji wa Mashamba ya Serikali ambapo jumla ya shilingi bilioni 0.21 zimekadiriwa kukusanywa.

Pia, inatarajiwa kuongezeka kwa idadi ya sera na miongozo itakayotolewa kutoka sita (6) hadi kumi na saba (17), na kuimarika kwa taarifa za kifedha kutoka kumi na nane (18) hadi ishirini na tano (25).

Ongezeko la mapato hayo linasababishwa na kuimarishwa kwa ufuatiliaji na usimamizi wa utekelezaji wa Mashirika ya Uwekezaji wa Umma na Taasisi za Umma, kuongezeka kwa idadi ya Mashirika ya Uwekezaji wa Umma, utekelezaji wa shughuli za ufuatiliaji, tathmini, uhakiki na tathmini ya mali za umma, tathmini ya matumizi ya mali za umma, pamoja na kuimarisha usimamizi wa kifedha kutoka Taasisi za Uwekezaji wa Umma.

Kukuza uwezo wa taasisi na uthabiti wake ambapo Ofisi inatarajia kukuza uwezo wa usimamizi wa mashirika ya umma ili kuimarisha utoaji wa huduma bora kwa kuongeza idadi ya wafanyakazi watakaofunzwa kwenye kozi fupi za kitaalamu kutoka wanne (4) hadi kufikia thelathini (30), na kuongeza idadi ya wafanyakazi watakaopatiwa kozi ndefu za

*INAENDELEA UK. 4*

# Dkt. Mwinyi shujaa wa ujenzi wa mashirika imara ya umma Zanzibar

*INATOKA UK. 3*

kitaaluma kutoka watano (5) hadi kufikia kumi (10).

Pia, inatarajia kuanzisha jumla ya miongozo sita (6) ya kiutendaji, kuongeza ujuzi wa watendaji katika masuala mtambuka hadi kufikia watendaji arobaini (40), na kuongeza asilimia ya wafanyakazi watakaopimwa katika hatua za kuimarisha utendaji. Ongezeko hili litatokana na kupatikana kwa mafunzo ya kitaalamu kwa wafanyakazi, kuanzishwa kwa kanuni na miongozo ya kiutendaji, uhamasishaji wa masuala mtambuka, pamoja na kutoa mafunzo ya kikazi na kuwaambatisha watendaji katika mafunzo ya kivitendo.

Kuendeleza ushirikiano na Taasisi za Umma na wadau wengine kutokana na uwepo wa jitihada za kuendeleza ushirikiano na taasisi nyingine na wadau, Ofisi inatarajia kutoa huduma na taarifa zenye ubora na kwa wakati, ambapo kwa sasa asilimia ya taarifa na huduma kamili zilizotolewa ni 20, na matarajio ni kufikia jumla ya taarifa 70 zitakazotolewa na kuhudumiwa.

Ofisi ya Msajili wa Hazina inatarajia kuimarisha hati za mashirikiano na taasisi nyingine kwa kuongeza idadi ya hati hizo kutoka mbili (2) za sasa hadi kufikia kumi (10), pamoja na kuongeza mikutano ya mashauriano kutoka kumi (10) hadi arobaini na minane (48).

**Uimarishaji huu utafikiwa kupitia maboresho ya huduma za mtandao, kuongeza taarifa za data, kuimarisha kituo cha taarifa, kuboresha usalama wa mfumo uliopo, na kuongeza kiwango cha moduli pamoja na vipengele vipya vya moduli.**

Ili kutimiza mipango hiyo, Ofisi inapanga kufanya mikutano na wadau muhimu, kuandaa mifumo imara ya upatikanaji wa taarifa, na kuandaa hati za Makubaliano ya Uelewano (MoUs) na wadau kwa mujibu wa matarajio ya kuimarisha mikakati iliyowekwa.

Kuwa na Mifumo ya kidijitali katika usimamizi wa mali za umma na uwekezaji wa Mashirika ya umma: Matarajio ni kuwepo kwa huduma za mifumo imara na inayoaminika ya kidijitali kwa ajili ya usimamizi wa Mali za Umma na Uwekezaji wa Mashirika ya Umma, kwa kuongeza idadi ya watendaji wa kiufundi katika eneo la ICT na kuwajengea uwezo kutoka watendaji wanne (4) hadi wanane (8), pamoja na kuboresha miundombinu ya TEHAMA.

Katika kuimarisha hatua za kitendaji, inatarajiwa kuimarishwa kwa mifumo ya usimamizi wa Mali za Umma na Uwekezaji wa Mashirika ya Umma ili kuhakikisha kuwa taarifa zinazoingizwa katika mifumo ni za uhakika na zinakidhi viwango, kutoka asilimia 10 hadi angalau asilimia 75.

Uimarishaji huu utafikiwa kupitia maboresho ya huduma za mtandao, kuongeza taarifa za data, kuimarisha kituo cha taarifa, kuboresha usalama wa mfumo uliopo, na kuongeza kiwango cha moduli pamoja na vipengele vipya vya moduli.

Kufanya ufuatiliaji, tathmini, ukaguzi wa ndani na uchambuzi: Katika hatua za kuimarisha ufuatiliaji, tathmini, ukaguzi na uchambuzi wa taarifa za Mashirika ya Uwekezaji wa Umma na Usimamizi wa Mali za Umma, Ofisi inapaswa kuhakikisha kuwa inaongeza ubora wa kazi zinazotekelezwa.

Hii inajumuisha kufuatilia idadi ya Taasisi za Umma zilizofanyiwa tathmini kwa kuzingatia viwango vya ubora, pamoja na kubaini asilimia ya taasisi ambazo hazijakidhi matakwa ya mfumo uliowekwa. Vilevile, inahitajika kuweka vigezo vya kupima wastani wa tathmini ya uondoaji wa mali za umma katika Taasisi za Umma.

Hivyo, mikakati hii imeweka msingi wa mageuzi ya kina kwa mashirika ya umma, ikilenga kuongeza mapato, kuboresha utendaji, kuimarisha uwajibikaji, kupunguza mianya ya rushwa na kuhakikisha rasilimali za umma zinatumika ipasavyo. Kupitia TEHAMA rasilimali watu, utawala bora na ufuatiliaji makini, serikali inatarajia mashirika ya umma kuwa injini ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii.



# MATUKIO KATIKA PICHA

## Idara ya Mali yazidi kuwa msaada Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar











# MABORESHO YA OFISI YA MSAJILI WA HAZINA ZANZIBAR

**Na Waheed M. I. Sanya**



Mapinduzi matukufu ya Zanzibar yalikuwa ni tukio la kihistoria lililobadilisha mwelekeo wa kisiasa, kijamii na kiuchumi wa visiwa vya Zanzibar ( Unguja na Pemba).

Mapinduzi hayo yaliweka msingi wa kubomoa mifumo ya kibaguzi, ikamaliza unyonyaji wa rasilimali, na kukomboa mali za taifa ili zitumike kwa manufaa ya wananchi wote bila ubaguzi.

Miongoni mwa misingi mikuu ya mapinduzi hayo ni umiliki, usimamizi na matumizi ya mali za umma kwa niaba ya wananchi ili kuhakikisha rasilimali za Zanzibar zinaendelea kuwa chini ya serikali ya wananchi na zinatumika kwa maendeleo sawa na shirikishi.

Lengo lilikuwa na dhana yenye mambo mengi ya kuhakikisha kwamba watu binafsi na jamii zote, hasa wale ambao wametengwa kihistoria, wanaweza kushiriki, kuchangia, na kufaidika kutokana na ukuaji wa kiuchumi, kijamii.

Miaka 62 ya Mapinduzi , Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeendelea kwa nguvu zote kutekeleza mageuzi makubwa katika sekta nyingi.

Hizi ni pamoja na mifumo ya kiutawala, kiuchumi na kisheria inayoendana na mahitaji ya sasa, sambamba na kuhifadhi misingi mikuu ya Mapinduzi. Ni katika muktadha huu wa kihistoria na kimapinduzi, kuanzishwa kwa ofisi ya Msajili wa Hazina mwaka 2021 kupitia Sheria ya Usimamizi wa Mali za Umma Namba 6, inapaswa kutazamwa kama muendelezo wa Mapinduzi na hatua madhubuti ya kuendeleza na kuimarisha usalama wa wananchi wa Zanzibar.

### KUANZISHWA KWA OFISI YA MSAJILI WA HAZINA ZANZIBAR

Kuanzishwa kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar mwaka 2021 kupitia Sheria namba 6 ya Usimamizi wa Mali za Umma kuliashiria hatua kubwa ya mageuzi ya kiutawala na udhibiti sahihi na bora wa mali za Serikali.

Sheria hii ilichukua nafasi ya Sheria ya Uwekezaji wa Umma namba 4 ya mwaka 2002, ambayo kwa miaka 19 ilikuwa inasimamia usimamizi wa uwekezaji wa umma na mashirika ya umma.

Marekebisho haya yalilenga kuimarisha uwazi, ufanisi, utendaji wa uwekezaji, na uwajibikaji katika taasisi zote zinazomilikiwa na serikali, kwa kuzingatia falsafa ya kimapinduzi ya kuhakikisha kuwa mali ya umma inaleta manufaa yanayoonekana kwa wananchi wake.

Maono ya Ofisi ni kuwa taasisi bora katika kudhibiti Mashirika ya Uwekezaji wa Umma na kusimamia mali za umma ndani ya Afrika Mashariki.

Dhamira yake ni kuanzisha na kusimamia mifumo ya usimamizi wa uwekezaji wa umma na mali ya umma kupitia miongozo ya kina, wafanyakazi wenye ujuzi stadi, na mfumo bora wa habari wa usimamizi ili kufikia matokeo yanayokusudiwa ya kiuchumi na kijamii.

### HISTORIA YA USIMAMIZI WA MALI ZA SERIKALI BAADA YA MAPINDUZI

Mapinduzi ya 1964 yalipoanza hadi pale marekebisho ya sasa yalipoanzishwa, usimamizi wa mali za serikali ulipitia idara mbalimbali, zikiwemo Hazina na Idara ya Uhakiki wa Mali.

Hatua hizi zinalenga kulinda mali ambazo pia zilitaifishwa baada ya Mapinduzi na kuhakikisha zinatumika kwa maslahi ya wananchi.

Mnamo 2005, Idara ya Uthibitishaji wa Mali iliunganishwa na uwekezaji wa umma ili kuongeza ufanisi katika kusimamia rasilimali za serikali.

Hatua hii iliweka msingi madhubuti wa kuanzisha mfumo mmoja na thabiti wa usimamizi wa mali, na hivyo kuhitimishwa na kupitishwa kwa sheria mpya ya 2021, ambayo inawakilisha kilele cha mageuzi yaliyoanzishwa na Mapinduzi.

### MAJUKUMU YA MSAJILI WA HAZINA ZANZIBAR

Kwa mujibu wa **Msajili wa Hazina Zanzibar, Waheed Muhammad Ibrahim Sanya**, kazi za msingi za Msajili ni pamoja na kusimamia uwekezaji, kutathmini utendaji wa mashirika ya umma, kudhibiti utoroshwaji wa mali, na kuishauri Serikali kuhusu gawio.

Alisema ofisi hiyo pia ina jukumu la kutoa miongozo ya utendaji kazi, kupitia upya miundo ya taasisi, na kushughulikia mikataba ya viongozi wa mashirika ya umma.

### IDARA YA UWEKEZAJI WA UMMA

Alibainisha kuwa idara hii ni kiungo muhimu kati ya serikali na mashirika ya umma kwa kuratibu sera za uwekezaji na kuimarisha utendaji wa kitaasisi.

Idara inaongozwa na vitengo viwili: uwekezaji wa umma na mifumo ya utawala pamoja na usimamizi wa ustawi.

Majukumu yake ni pamoja na

**MIAKA 62**

**Ya Mapinduzi , Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeendelea kwa nguvu zote kutekeleza mageuzi makubwa katika sekta nyingi.**

kuandaa miongozo ya usimamizi, kuandaa mikataba ya utendakazi, na kushauri njia bora za kuongeza mtaji kwa mashirika ya umma.

Idara hufanya uchambuzi wa bajeti za mashirika, kufuatilia miradi, na kutoa ushauri juu ya malipo ya mafao na motisha kwa wafanyikazi.

Aidha alieleza kuwa Idara pia inasimamia ufuatiliaji wa mikataba ya utendaji kazi, mipango mkakati, na uboreshaji wa ufanisi wa kifedha ndani ya mashirika.

Kupitia idara hii, Ofisi ambayo inafuraha kwa kuungwa mkono na ushirikiano kamili wa taasisi za umma imeimarisha usimamizi wa vitega uchumi vya umma na kuongeza uwezo wa mashirika kuchangia hazina ya kitaifa hasa kupitia gawio (ikiwa ni kutengeneza faida) na utumaji wa mapato ya lazima yasiyo ya kodi, ambayo yanasimamiwa na mifumo maalum ya kisheria.

Msajili wa Hazina anasimamia michango hii na kuhakikisha utiifu.

Ofisi imetayarisha Mpango Mkakati wa 2025/2026–2027/2028, unaoeleza mwelekeo mpya kwa mashirika ya umma katika uchumi wa kisasa, unaojengwa juu ya kanuni za Mapinduzi.

## IDARA YA USIMAMIZI NA USAJILI WA MALI ZA UMMA

Idara hii inajumuisha mgawanyiko wa usimamizi, usajili wa mali, na Uondoaji wa Mali ya Umma.

Ina jukumu la kusimamia sera, kufanya tathmini, kutunza kumbukumbu, kusajili mali, na kuratibu uondoaji wa mali zilizopitwa na wakati.

Idara pia hufanya ukaguzi wa mali, kuidhinisha rejista za mali, na kuhakikisha kuwa uuzaji wa mali za serikali unafuata taratibu zinazofaa na mapato yanatumwa serikalini.

Aidha alieleza kuwa Idara imeimarisha mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), imeanzisha Mfumo wa Usajili wa Mali za Serikali (ZGAMIS), na kusajili zaidi ya mali 23,638 zenye thamani ya TZS 262 bilioni.

Mpango huu umeongeza uwazi, kupunguza upotevu wa mali, na kuimarisha uwajibikaji ndani ya taasisi za umma, na hivyo kuendeleza lengo la kimapinduzi la kulinda rasilimali za taifa.

## MAFANIKIO YA OFISI YA MSAJILI WA HAZINA

Ofisi imeboresha usimamizi wa mali zilizopitwa na wakati na kukusanya zaidi ya TZS 1.025 bilioni kutokana na matumizi yao.

Miongozo mbalimbali ya usimamizi wa shirika imeandaliwa, ikiwa ni pamoja na hati za bodi, miongozo ya tathmini ya mradi,

**TZS 262 BILIONI**

**Aidha alieleza kuwa Idara imeimarisha mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), imeanzisha Mfumo wa Usajili wa Mali za Serikali (ZGAMIS), na kusajili zaidi ya mali 23,638 zenye thamani ya TZS 262 bilioni.**

mifumo ya bajeti, na miongozo ya mipango ya kimkakati.

**Bwana Sanya** ,Akizungumzia masuala ya ICT, alisema kuwa mifumo imeimarishwa kupitia (OTRMIS), tovuti mpya, na mfumo wa utupaji mali mtandaoni ambao unakaribia kukamilika.

Mapato ya gawio kutoka kwa mashirika ya uwekezaji yaliongezeka kutoka TZS 8.6 bilioni (2020/21) hadi TZS 13.05 bilioni (2022/23).

Kwa mwaka wa fedha 2025/26, serikali inatarajia kukusanya TZS 25 bilioni kutoka kwa gawio na michango ya mashirika ya umma.

## CHANGAMOTO

Alisema changamoto zinazohitaji ufumbuzi ni pamoja na uhaba wa watumishi na ukosefu wa wataalamu waliobobea hasa katika Idara ya Mashirika na Idara ya Mali.

Alibainisha kuwa baadhi ya taasisi zinashindwa kuwasilisha taarifa kwa wakati, huku nyingine zikiwa na uwezo mdogo wa kutunza kumbukumbu za mali.

Bajeti chache za ukaguzi, ukosefu wa rasilimali, na matukio ya matumizi mabaya ya mali bado ni changamoto katika usimamizi wa mali.

Changamoto nyingine ni pamoja na kutotosha kwa matokeo ya uthamini wa mara kwa mara katika taarifa zisizo kamili kuhusu thamani ya mali za serikali.

Marekebisho hayo ambayo yanaongozwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar, yameleta kasi mpya katika usimamizi wa mali za umma, uwekezaji, uwazi na uwajibikaji.

_Wakati Zanzibar inaadhimisha Miaka 62 ya Mapinduzi, mafanikio hayo yanadhihirisha kuwa Mapinduzi si tukio la kihistoria tu, bali ni mchakato endelevu wa kujenga uchumi imara, kusimamia rasilimali za umma, na kuhakikisha kuwa wananchi wananufaika na mali zao.

Hivyo, kwa kuimarisha mifumo, kuongeza mapato, na kujenga taasisi imara, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kutafsiri malengo ya Mapinduzi ya 1964 kwa vitendo na kuweka msingi imara wa uchumi imara na ustawi wa Taifa.

***Tunawatakia heri ya Mwaka Mpya 2026!!!***



# MATUKIO KATIKA PICHA










# MAFANIKIO MIAKA MITANO YA DKT. MWINYI 2020-2025

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi amekuwa mstari wa mbele katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM Zanzibar kwa mwaka 2020-2025 kwa kusimama imara kufanikiwa kukuza uchumi wa wananchi, kuboresha sekta ya elimu, afya, maji, nishati na uchumi wa buluu.

## SEKTA YA UCHUMI

Rais Dk. Mwinyi amewezesha kukua kwa uchumi wa Zanzibar kutoka asilimia 5.1 kwa mwaka 2021 na kufikia asilimia 7.1 kwa mwaka 2024 kutokana na sababu mbali mbali zikiwemo.

Sababu hizo ni pamoja na kuimarika kwa mazingira ya biashara na uwekezaji; Kuongezeka kwa uingiaji wa watalii nchini; Kuongezeka kwa miradi ya uwekezaji na nyenginezo (kwa maelezo zaidi rejea ukurasa wa 4 na 5).




## SEKTA YA AFYA



Serikali ya Zanzibar imeboresha Sekta ya Afya baada ya kukamilisha ujenzi wa Hospitali 10 za Wilaya na Hospitali 1 ya Rufaa ya Mkoa wa Mjini Magharibi kwa kuhakikisha hospitali zote zina madaktari bingwa, dawa, vitendea kazi na vifaa tiba.

Hospitali zote zinaendelea kutoa huduma bora kwa wananchi na kuunganishwa na mifumo inayopokea rufaa za wagonjwa kutoka ngazi ya Huduma za Afya za Msingi hadi Hospitali kuu kwa lengo la kurahisisha matibabu kwa wananchi wote wa Unguja na Pemba.

## SEKTA YA ELIMU




Serikali imesimamia na kutekeleza moja ya Sera ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya kutoa elimu bila ya malipo kuanzia ngazi ya Maandalizi hadi Sekondari. Imekamilisha ujenzi wa shule (skuli) za msingi 37 na skuli 23 za Sekondari Unguja na Pemba.

Imewezesha kuongezeka kwa kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi wa Kidato cha Nne kutoka asilimia 66.3 mwaka 2021 hadi asilimia 82 mwaka 2024; kwa upande wa Kidato cha Sita ufaulu kutoka asilimia 98.8 mwaka 2021 na kufikia asilimia 99.9 mwaka 2024.

SMZ imeanzisha Mfumo wa Usimamizi wa Shule (School Information System) unaowezesha ukusanyaji wa taarifa za idadi ya watumishi na wanafunzi, matokeo ya wanafunzi, mahudhurio ya walimu na wafanyakazi kwa wakati.

Kiwango cha wanafunzi walionufaika na mikopo ya Elimu ya Juu kupitia Mfuko wa Mikopo wa Elimu ya Juu ya Zanzibar, kimeongezeka kutoka wanafunzi 4,045 na kufikia wanafunzi 11,495 ambayo ni sawa na asilimia 164 ya shabaha ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi.

## SEKTA YA MAJI



Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeboresha huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wake kwa kuboresha miundombinu ya maji; kutekeleza miradi ya kimkakati ya maji; kuimarisha ushirikiano na wadau wa maendeleo; na kuboresha usimamizi wa rasilimali za maji.

Hatua hizi zimewezesha kupatikana kwa huduma ya maji safi na salama katika Shehia zote 388 za Zanzibar (Unguja Shehia 260 na Pemba 128) na kufikia asilimia 88.22 ya uzalishaji wa maji na kusaidia kupunguza changamoto ya upatikanaji wa maji safi na salama.

## SEKTA YA NISHATI YA UMEME



Serikali imeboresha upatikanaji wa huduma ya umeme kwa wananchi kwa kuvifikia vijiji 231 (Unguja 144 na Pemba 87) sawa na asilimia 76 ya vijiji 305 vilivyotakiwa kuunganishiwa huduma hiyo. Aidha, kwa mwaka 2024, jumla ya wateja 138,065 wameunganishiwa huduma ya umeme Unguja na Pemba.

Aidha, serikali imejenga kilomita 98.05 kati ya kilomita 100.13 zilizopangwa kujengwa kwa njia ya umeme mkubwa (HT) ambazo sawa na asilimia 107 na kilomita 73.4 kati ya kilomita 81 zilizopangwa kujengwa kwa njia ya umeme mdogo (LV) ambazo ni sawa na asilimia 91.



## BANDARI

Rais Dk. Mwinyi ameimarisha ujenzi wa Bandari ya Mafuta na Gesi katika eneo la Mangapwani kwa kutoa vitalu ambavyo vitaenda kujengwa sehemu ya kuhifadhia mafuta na gesi pamoja na kujengwa jetty maalum kwa ajili ya ushushaji wa bidhaa hiyo.

SMZ imeimarisha pia Bandari za Mkoani, imejenga Bandari kavu mpya katika eneo la Maruhubi, imeimarisha Bandari ya Wesha, imekamilisha ujenzi wa Bandari ya Fumba na imeimarisha Bandari ya Malindi na inaendelea na ujenzi wa Bandari Shumba Kisiwani Pemba.

Kuimarika kwa miundombinu hiyo, kumepelekea kuongeza ufanisi katika Sekta ya Bandari na kupelekea wafanyabiashara wanaozitumia bandari hizi kufanya biashara zao kwa wepesi na ufanisi (kwa maelezo zaidi rejea ukurasa wa 24, 25 na 26).

## UTALII



Uandaaji wa filamu na Makala ya kuutangaza utalii Tanzania (The Royal Tour) iliyoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kushirikiana na Rais Dk. Mwinyi kumeweza kuvitangaza vivutio vya utalii vya Bara na Visiwani na kuleta mafanikio makubwa kupitia sekta hiyo.




## UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, imeimarisha Taasisi na Mifuko mbali mbali ya uwezeshaji wananchi kiuchumi, programu za mafunzo ya ujasiriamali, upatikanaji wa mikopo nafuu na uanzishaji wa vikundi vya kiuchumi katika sekta za kilimo, uvuvi, ufugaji, biashara ndogo ndogo na viwanda.

Serikali imetoa mikopo isiyo na riba ya Shilingi 3,584,300,000 kwa wawekezaji wa ndani 38 ambao umezalisha ajira 438 na imewezesha upatikanaji wa ajira 233,615 kati ya ajira 300,000 zilizoahidiwa. Ajira hizi zimewasaidia sana wananchi katika kumudu mahitaji yao ya lazima ya kila siku ikiwemo; chakula, mavazi; matibabu na malazi.

 *"USIMAMIZI IMARA WA MALI NA MASHIRIKA YA UMMA KWA MAENDELEO ENDELEVU"*

## BARABARA



Katika juhudi za kuimarisha miundombinu ya Barabara, Serikali imeendelea na ujenzi wa zaidi ya kilomita 675.9 za barabara kwa Unguja na Pemba. Ujenzi wa barabara hizo unaendelea kurahisisha mawasiliano pamoja na usafirishaji wa bidhaa na kupelekea kuongezeka kwa pato la nchi na pato la mtu mmoja mmoja.

## USAFIRI WA ANGA




Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeimarisha viwanja vya Ndege kikiwemo Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume pamoja na ukarabati wa majengo ya abiria ya Terminal 1 na 2 na kusaidia kukua kwa mapato.

Mapato yameongezeka na kufikia shilingi bilioni 40.2 kwa mwaka 2025 kutoka shilingi Bilioni 12.9 kwa mwaka 2021, sawa na ongezeko la asilimia 211.6. Abiria nao wameongezeka kutoka 840,559 kwa mwaka 2020 na kufikia 2,140,956 kwa mwaka 2025.

Kwa upande wa Kiwanja cha Ndege cha Pemba, Serikali imekamilisha kazi za awali za ujenzi wenye thamani ya Euro 170. Haya yanafanyika ikiwa ni kutekeleza kwa vitendo Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi.

## UCHUMI WA BULUU

Serikali imetoa umuhimu wa kipekee katika Sekta ya Uchumi wa Buluu kwa kuchukua hatua mbali mbali zikiwemo utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia; kukamilisha Sera ya Uchumi wa Buluu ya mwaka 2022; Sera ya Uvuvi; Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mali Asili za Baharini pamoja na ujenzi wa madiko na masoko ya samaki. Hatua hizo zimepelekea mafanikio mbali mbali.

Kwa upande mwengine, uzalishaji wa zao la mwani umeongezeka kutoka Tani 8,785 zenye thamani ya Shilingi Bilioni 5.3 kwa mwaka 2020 hadi kufikia Tani 19,716 zenye thamani ya Shilingi Bilioni 16.1 kwa mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 124.6.

Mafanikio haya yote yanawawezesha wananchi kumudu mahitaji yao ya kila siku pamoja na upatikanaji wa lishe ya uhakika (kwa maelezo zaidi rejea ukurasa wa 31, 32 na 33).





## UWEKEZAJI

Serikali umesimamia upatikanaji wa wawekezaji katika visiwa 15 kati ya visiwa 21 kwa awamu ya kwanza. Kupitia wawekezaji hao, Serikali imekamilisha uwekezaji wa Kisiwa cha Bawe na kuanza shughuli zake na visiwa tisa (9) kikiwemo cha Pamunda vinaendelea na ujenzi.

Kukamilika kwa uwekezaji katika visiwa hivyo kutapelekea kuongezeka kwa pato la nchi yetu ambalo litasaidia katika ujenzi wa miundombinu na kuimarisha maisha ya wananchi.




Zanzibar imeimarisha mifumo ya hifadhi ya jamii kupitia Taasisi zake ikiwemo Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), ambao hutoa huduma za mafao kwa wafanyakazi na wastaafu, Serikali imeongeza kiwango cha malipo ya Pencheni Jamii.

Pencheni hizo ni kwa wazee waliofikia umri wa miaka 70 kutoka Shilingi 20,000 kwa mwaka 2015/2016 hadi kufikia Shilingi 50,000 kwa mwaka 2023/2024 sawa na ongezeko la asilimia 150.

Pia, serikali imeandaa utaratibu maalum wa kutoa Fao la Matibabu ambalo litasimamiwa na Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar (ZHSF). Haya yote yanafanyika kwa lengo la kuwapunguzia wananchi ukali wa maisha (kwa maelezo zaidi rejea ukurasa wa 28, 29, 49 na 50).

## MABORESHO YA MASLAHI YA WATUMISHI WA UMMA




Serikali imefanya marekebisho ya Mshahara kwa Watumishi wote wa Serikali na kupelekea ongezeko la Shilingi 48,329,458,032 kutoka Shilingi 35,514,281,480 kuanzia Juni mwaka 2021 hadi Julai 2022 ikiwa ni tofauti ya Shilingi 12,815,239,552 sawa na asilimia 36.

Kuongezwa kwa posho ya Likizo kwa Watumishi wa Umma wa kawaida kutoka Shilingi 100,000 hadi Shilingi 200,000 na Wateule kutoka Shilingi 300,000 hadi 1,000,000 na 3,000,000 kuanzia Mwezi Julai, 2024.

Lengo ni kuhakikisha kila mtumishi wa umma anamudu mahitaji yake ya msingi na kumuwezesha kufanyakazi kwa uweledi na ufanisi.

## KUDUMISHA MUUNGANO



Katika kuendeleza tunu ya Taifa iliyoasisiwa na Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Julius Kambarage Nyerere na Rais wa Zanzibar Hayati Sheikh Abeid Amani Karume, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbali mbali za kuimarisha Muungano wetu ikiwemo kufanya vikao 23 vya kujadili masuala ya Muungano.

Vikao hivyo, vimefanikisha kuondoa Hoja 15 za Muungano. Muungano umeendelea kuimarishwa kupitia vikao vya mashirikiano baina ya Taasisi za SJMT na SMZ kupitia vikao 148 vya ushirikiano kwa kujadili masuala yanayoshabihiana. Wananchi wa pande mbili za Muungano wameendelea kuishi kwa pamoja bila ya kujali dini, kabila au eneo mtu analotoka.

Hivyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanikiwa kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa kipindi cha miaka mitano kwa mafanikio makubwa ikiwa ni kuhakikisha inatekeleza maagizo na maelekezo ya Ilani hiyo.



# YAJAYO NI NEEMA ZAIDI, UONGOZI UNAOACHA ALAMA VIPAUMBELE MIAKA MITANO IJAYO YA DKT. MWINYI MADARAKANI



MIAKA mitano ijayo ya utawala wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi itakuwa na mafanikio makubwa kutokana na uwepo wa vipaumbele bora vinavyokwenda kumsaidia mwananchi mmoja mmoja.

Vipaumbele na mwelekeo wa mipango ya Serikali ya Awamu ya Nane katika kipindi cha miaka mitano imeelezwa kuwa na dhamira ya kutafsiri na kutekeleza Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya 2025 – 2030, mipango mikuu ya maendeleo.

Pia, vipaumbele hivyo vinakwenda kutekeleza ahadi zilizotolewa wakati wa kampeni za uchaguzi wa 2025 pamoja na kuendeleza mafanikio yaliyopatikana katika awamu zote za uongozi wa nchi yetu toka awamu ya kwana hadi sasa ya nane.

**AMANI NA UMOJA WA KITAIFA**

Kipaumbele muhimu cha Serikali ya Awamu ya Nane katika kipindi chake cha pili ni kuendelea kudumisha amani, umoja na mshikamano kama msingi mkuu wa maendeleo nchini.

Lengo likiwa ni kuzidi kuwaunganisha wananchi wa Zanzibar kuwa wamoja bila ya kujali rangi, imani ya dini, jinsia, asili ya mtu, au itikadi ya kisiasa, jambo ambalo litazingatiwa katika uteuzi wa viongozi na watendaji katika utumishi wa umma pamoja na kuwapatia fursa mbali mbali wananchi wote na kuhakikisha wanafaidika na huduma za Serikali kwa misingi ya usawa.

**KUCHOCHEA MAPINDUI YA UCHUMI WA KISASA NA ENDELEVU**

Ukuaji wa uchumi ni chachu ya kuleta maendeleo endelevu, na ustawi wa wananchi, Serikali katika kipindi hiki cha pili cha Awamu ya Nane imehakikisha kuleta ukuaji wa uchumi unafungamana na uimara wa sekta za uzalishaji.

Pia, kusaidia kuwepo kwa fursa za uwekezaji, upatikanaji wa mitaji na ushirikishwaji wa sekta binafsi. Katika kufikia dhamira hiyo, Serikali itaendelea kuimarisha hali ya uchumi kwa kuchukua hatua mbali mbali zikiwemo kuwajengea mazingira wezeshi wananchi wanaoishi kwa kipato cha chini ili kuwawezesha kujikimu kwa huduma za msingi.

Pamoja na mambo mengine, Serikali itachukua hatua za kudhibiti mfumuko wa bei kuwa chini ya asilimia 5 kwa mwaka, kuongoza ukuaji wa Pato la Taifa kutoka asilimia 7 hadi kufikia asilimia 10 kwa mwaka, kuzalisha fursa mpya za ajira laki tatu na nusu (350,000) na kuongeza kipato cha mwananchi kutoka Dola za Kimarekeni 1,241 (sawa na TZS 3,219,898.6) hadi Dola za Kimarekani 1880 (Sawa na TZS 4,877,848).

Serikali itaongeza usimamizi wa Sera za Uchumi, Fedha na Mapato kwa kuimarisha mifumo ya kifedha na upatikanaji wa mitaji ili kuimarisha uwekezaji na kuongeza ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

Kufanya mapitio ya Sera na Sheria zinazosimamia fedha ili kuboresha huduma za fedha, tutaimarisha ushirikiano na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika usimamizi wa Sera za fedha na kodi kwa kuzingatia mazingira maalum ya Zanzibar, kuimarisha na kusimamia upatikanaji wa mikopo ya masharti nafuu kwa wajasiriamali na vikundi vya kijamii, kuboresha upatikanaji wa huduma za kibenki kwa wananchi wa mijini na vijijini pamoja na kuimarisha matumizi ya mifumo ya kidijitali katika utoaji wa huduma za kifedha ili kupunguza matumizi ya fedha taslimu.

Serikali inatambua umuhimu wa Sekta Binafsi katika kuimarisha ukuaji wa uchumi na ustawi wa jamii. Serikali imedhamiria kuleta maendeleo ya nchi na wananchi kwa kuzidi kuyaimarisha mazingira ya biashara na kuhamasisha uwekezaji kwa kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi ili kuwa na uchumi shirikishi.

Serikali itaweka mazingira rafiki kwa sekta binafsi kwa kupunguza urasimu na kuweka vivutio vya uwekezaji, kuimarisha ushirikiano kupitia ubia wa sekta ya umma na binafsi (PPP), kutoa fursa kwa wajasiriamali kupitia mafunzo, mikopo nafuu na kuimarisha miundombinu ya masoko, kuhamasisha uwekezaji katika ubunifu na teknolojia za kisasa, kuendeleza sekta za kilimo, viwanda na huduma na kuweka mazingira ya kubaini fursa za ajira hususan kwa vijana na wanawake kupitia miradi ya maendeleo, ujasiriamali na kufanya uwekezaji katika viwanda vinavyoongeza thamani.

**UCHUMI WA BULUU**

Uchumi wa buluu unaojumuisha utalii, uvuvi, mafuta na gesi asilia, mazao ya baharini, kilimo cha mwani, bandari na biashara zinazohusiana na usafiri wa baharini ni sera kuu ya Serikali ya Awamu ya Nane. Katika kipindi cha pili cha uongozi, Serikali itaongeza jitihada za kuimarisha sekta za uchumi wa buluu ili kuchochea kasi ya kukuza uchumi wetu.

Katika utalii, Serikali imedhamiria kuongeza idadi ya watalii wa kimataifa wanaoitembeleza Zanzibar kutoka 800,000 hadi watalii 1,500,000 sambamba na kuongeza wastani wa matumizi ya siku kwa mtalii kutoka Dola za Kimarekani 418 mwaka 2024 hadi Dola 506 kwa siku.

# YAJAYO NI NEEMA ZAIDI, UONGOZI UNAOACHA ALAMA VIPAUMBELE MIAKA MITANO IJAYO YA DKT. MWINYI MADARAKANI

Aidha, imedhamiria kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea Pemba kutoka 200,000 hadi 300,000 kwa mwaka. Kuimarisha utalii wa mikutano ya kitaifa, kikanda na kimataifa, matamasha, utalii wa matibabu, maonyesho na michezo, kuongeza vyumba vyenye hadhi ya juu kutoka 7,626 hadi 10,000 ili kuvutia watalii wenye hadhi kubwa pamoja na kuibua na kuimarisha utunzaji wa vivutio vya utalii vya kimaumbile, mashamba ya viungo na maeneo ya Hifadhi za misitu kwa ushirikiano na wanajamii.

Uvuvi, mazao ya baharini na kilimo cha mwani ni sekta muhimu katika Uchumi wa buluu ambapo katika kipindi cha miaka mitano inayokuja, Serikali itaendeleza sekta hizo kwa kuimarisha miundombinu ya uvuvi kwa kujenga madiko na masoko makubwa mawili, Fungurefu kwa Unguja na Mkoani kwa Pemba pamoja na masoko madogo matano (5).

Serikali itajenga bandari kubwa mbili za uvuvi, eneo la Ngalawa kwa Unguja na Shumba Mjini kwa Pemba. Pia, itajenga viwanda vya kuchakata samaki na kununua meli kubwa za uvuvi.

Kwa upande wa mazao ya bahari, itahakikisha inawakuza wafugaji wa mazao ya bahari wakiwemo wafugaji wa samaki, matango bahari na kaa kwa kuwawezesha kufuga kibiashara na pia tutajenga mabwawa ya ufugaji wa samaki na vizimba vya kufugia samaki baharini.

Katika kilimo cha mwani, kutaongezwa uzalishaji wa mwani mkavu kutoka tani 19,715 mwaka 2024 hadi tani 40,000 kufikia mwaka 2030 pamoja na kuanzisha vituo saidizi vya kusarifu mwani ili kuuongeza ubora na thamani ya bidhaa zinazozalishwa kutokana na mwani.

Aidha, serikali itahakikisha inatatafuta fursa zaidi za masoko ya mwani na bidhaa zake ili kuwapa tija zaidi na faida wakulima wa mwani.

Kuhusu sekta ya mafuta na gesi asilia, jitihada zilizofanyika za kuimarisha sekta hizi zimeanza kupata mafanikio. Tayari Serikali imeshatangaza vitalu 10 vya mafuta na gesi asilia vikiwemo 8 vya baharini na viwili vya nchi kavu kwa wawekezaji wa utafutaji wa rasilimali hizo.

Serikali imekamilisha marekebisho ya modeli ya mkataba wa mgawanyo wa mapato ya uzalishaji kwa lengo la kuwavutia wawekezaji na kulinda maslahi ya nchi yetu.

Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, SMZ itahakikishja inalenga mambo mengi ikiwemo kuendeleza utafiti na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia, kuendelea kutangaza na kugawa vitalu vipya vya uwekezaji wa mafuta na gesi asilia na kujenga kituo cha kudumu cha kuhifadhi taarifa za sampuli za mafuta na gesi asilia.

Bandari na usafiri wa bahari vina umuhimu mkubwa kwa nchi za visiwa kama ilivyo Zanzibar. Serikali itaendeleza ujenzi wa bandari jumuishi ya Mangapwani inayojumuisha bandari ya mizigo, uhifadhi wa makontena, uhifadhi wa mafuta na gesi pamoja na uhifadhi wa nafaka.

Serikali itahakikisha inajenga bandari za kisasa za abiria Mpigaduri na Kizimkani kwa Unguja na Shumba na Wete kwa Pemba pamoja na kuimarisha bandari ya Malindi kwa ajili ya huduma za utalii.

Katika kuimarisha usafiri wa bahari, Serikali imeingia mkataba wa ujenzi wa boti 2 za kisasa za mwendo kasi zitakazofanya safari za kusafirisha abiria katika bandari za Unguja, Pemba, Tanga na Dar es salaam.

Lengo likiwa ni kuimarisha na kupanua wigo wa huduma za usafiri wa baharini ili kukuza biashara, kuongeza mapato na kurahisisha usafiri wa mizigo na abiria kati ya Zanzibar, Bara na nchi jirani.

### SEKTA ZA UZALISHAJI

Sekta za uzalishaji zina mchango mkubwa katika kuongeza uzalishaji, fursa za ajira na kukuza Pato la Taifa. Katika kipindi cha pili cha Serikali ya Awamu ya Nane, Serikali imedhamiria kuchukua hatua madhubuti za kuimarisha na kukuza maendeleo ya Sekta za Uzalishaji zikiwemo Kilimo, Mifugo, Maliasili na Viwanda.

Kwa kuzingatia umuhimu wa sekta za kilimo kwa maendeleo na ustawi wa uchumi, upatikanaji wa chakula na kipato kwa wananchi wengi wa Zanzibar hasa wanaoishi vijijini, Serikali ina dhamira ya kuongeza uzalishaji na huduma katika sekta ya Kilimo ikiwemo kufanya mageuzi makubwa yanayozingatia matumizi ya teknolojia ya kisasa ili kuongeza uzalishaji na tija katika kilimo.

Uimarishaji wa miundombinu ya uzalishaji, ikiwemo mifumo ya umwagiliaji, upatikanaji wa mikopo nafuu na masoko kwa bidhaa za kilimo.

Serikali itaanzisha hifadhi ya Taifa ya chakula kwa kukarabati maghala manne 4 na kujenga vihenge (Silos) Dunga Unguja na Chamanangwe Pemba vyenye uwezo wa kuhifadhi tani 60,000 kwa wakati mmoja.

Serikali, pia itaanzisha mfumo wa upatikanaji wa huduma za pembejeo muhimu za kilimo ikiwemo mbolea, viatilifu, mbegu na miche bora, huduma za ugani na zana za kisasa za kilimo kwa kushirikiana na sekta binafsi.

Serikali itaandaa program maalum ya kuongeza uzalishaji wa mazao ya karafuu, matunda, mboga na viungo kwa kuwahusisha vijana na kuimarisha upatikanaji wa masoko ya bidhaa za kilimo ndani na nje ya nchi.

Serikali imedhamiria kuchukua hatua za kuimarisha Sekta ya mifugo kutokana na umuhimu wake kiuchumi kwa kuwezesha matumizi ya teknolojia za kuongeza uzalishaji na tija, kuimarisha miundombinu ya uzalishaji na upatikanaji wa mikopo nafuu na masoko ya bidhaa za mifugo.



# YAJAYO NI NEEMA ZAIDI, UONGOZI UNAOACHA ALAMA VIPAUMBELE MIAKA MITANO IJAYO YA DKT. MWINYI MADARAKANI




SMZ itaongeza uzalishaji wa kuku, mayai, nyama na kulinda masoko ya bidhaa hizo kwa kudhibiti uingizaji wa bidhaa za mifugo kutoka nje ya nchi.

Ushirikiano na sekta binafsi, Serikali itaweka vivutio katika uanzishaji wa viwanda vya uzalishaji wa vifaranga na vyakula vya mifugo. Pia, itahakikisha inajenga vituo vya kisasa vya matibabu ya mifugo na kutoa ushauri wa kitaalamu wa ufugaji katika kila Wilaya pamoja na kuwezesha vijana kushiriki katika ufugaji kwa kuwapatia taaluma, mikopo yenye masharti nafuu na masoko.

Misitu na maliasili ni rasilimali muhimu kwa maendeleo ya Zanzibar na watu wake. Kwa kuzingatia hilo, Serikali itachukua hatua za makusudi kulinda na kusimamia maliasili na misitu yetu kwa matumizi endelevu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

Lengo la kufikia dhamira hiyo, Serikali itaongeza ushiriki wa jamii katika udhibiti na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu kwa kuongeza misitu mipya ya hifadhi, kuongeza vivutio katika maeneo ya uhifadhi na kuboresha miundombinu ya huduma.

Pia, Serikali itatekeleza mpango wa kurithisha Zanzibar ya kijani kwa kupanda miti ya aina mbali mbali ya matunda, bustani, miti ya vivuli, mikoko na miti ya asili, kuwezesha vijana kwa mitaji na taaluma katika kuzalisha na kusarifu asali kibiashara pamoja na kuandaa programu za kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia itayozingatia utoaji wa ruzuku katika bei na vifaa vya nishati safi.

Lengo ni kusaidia wananchi kujenga uwelewa juu ya umuhimu wa kutumia nishati safi na usalama wake. Serikali inathamini mchango wa vyama vya ushirika vikiwemo vya uzalishaji na SACCOS katika kukuza uchumi na kuinua kipato cha wananchi katika kujikimu kimaisha.

Kwa kuzingatia umuhimu huu, Serikali itaanzisha mifumo ya kielektroniki kurahisisha usajili, usimamizi na ukaguzi wa vyama vya ushirika, kupata masoko ya uhakikia, kuhamasisha vyama vya ushirika kununua hisa katika benki ya Ushirika Tanzania na kuweka vivutio maalum kwa lengo la kuongeza ushiriki wa vijana na makundi mengine katika sekta ya ushirika.

**NISHATI**

Upatikanaji wa nishati ya umeme, mafuta na gesi wenye kukidhi mahitaji muhimu katika kuchochea uzalishaji na upatikanaji endelevu wa huduma na ukuaji wa uchumi, ni mambo ya msingi yaliyopewa mazingatio katika kipindi cha pili cha uongozi wa Serikali ya Awamu ya Nane.

Katika kufikia malengo hayo, Serikali imedhamiria kujenga miundombinu ya kisasa ya uzalishaji wa umeme kutokana na vyanzo vipya ikiwemo jua, upepo na umeme unaotokana na taka ili kupunguza utegemezi wa chanzo kimoja.

Aidha, kutajengwa vituo maalum vya gesi na umeme na kushajiisha matumizi ya magari maalum yanayotumia nishati ya umeme, kujenga miundombinu ya uhifadhi wa mafuta na gesi asilia na kuendeleza ushirikiano na sekta binafsi katika kuhakikisha upatikanaji wa mafuta unaozingatia uhimilivu wa bei na uwezo wa wananchi.

Serikali itaongeza matumizi ya nishati mbadala katika sekta ya kilimo, huduma za maji, elimu na afya.

Sekta ya biashara ina umuhimu mkubwa katika mipango yetu ya maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii kwa kuchangia katika mzunguko wa fedha, fursa za ajira na upatikanaji wa bidhaa na huduma. Serikali katika kipindi hiki imedhamiria kuimarisha sekta ya biashara kwa kuchukua hatua mbali mbali zikiwemo kuimarisha urari wa biashara katika uchumi wa Zanzibar.

Aidha, SMZ itajenga kituo cha Kimataifa cha Biashara Dimani, kuendeleza program ya mapitio ya ada na tozo ambazo ni kero kwa wananchi na wafanyabiashara, kudhibiti uingizaji wa bidhaa bandia kwa kuimarisha usimamizi kwenye vituo vya ukaguzi wa bidhaa na kujenga maabara za kisasa za upimaji (Testing House) Chamanangwe Pemba na Dunga ikiwa na lengo la kudhibiti ubora wa bidhaa zinazoingizwa na kuzalishwa hapa nchini.

Katika kuimarisha sekta ya viwanda yenye umuhimu mkubwa katika kukuza uchumi, kuongeza uzalishaji wa bidhaa na kuleta ajira, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imedhamiria kuchukua hatua za kuandaa programu maalum ya kukuza viwanda vya usindikaji wa bidhaa zinazotokana na mazao yenye thamani (high value crops) ikijumuisha viungo, mafuta ya mimea na mwani, kuongeza mchango wa sekta ya viwanda katika Pato la Taifa kutoka asilimia 20.8 ya sasa hadi asilimia 25, kuweka mkakati wa kuongeza viwanda vipya ili kupunguza uingizaji wa bidhaa kutoka nje kwa bidhaa maalum na kukidhi asilimia 60 ya mahitaji ya ndani.

Serikali pia itayaendeleza maeneo maalum ya uwekezaji wa viwanda (EPZ) ya Chamanagwe Pemba na Dunga Unguja kwa kuweka miundombinu muhimu ya uzalishaji na kuwawezesha wazalishaji wadogo kuyatumia maeneo hayo.

Aidha, Serikali itawawezesha wawekezaji wa ndani katika kuzalisha vifungashio bora vya bidhaa kwa lengo la kukidhi mahitaji ya soko la ndani hapa nchini.

Ardhi ni rasilimali muhimu kwa shughuli mbali mbali za maendeleo ikiwemo kilimo, viwanda, hifadhi ya mazingira na uwekezaji. Serikali itahakikisha inasimamia vyema na kwa ufanisi sera na sheria za matumizi ya ardhi ndogo tuliyonayo kwa matumizi endelevu ya maendeleo. Katika kufikia dhamira hiyo, Serikali itaendelea kufanya mapitio ya sera, mipango na sheria

# YAJAYO NI NEEMA ZAIDI, UONGOZI UNAOACHA ALAMA VIPAUMBELE MIAKA MITANO IJAYO YA DKT. MWINYI MADARAKANI

za ardhi ili kwenda sambamba na mabadiliko ya kijamii, kiuchumi, kimazingira na utekelezaji wa mkakati wa usimamizi wa ardhi.

Serikali itaendeleza upimaji na kuyatangaza maeneo maalum ya kuduma ya ardhi kwa matumizi ya viwanda na uwekezaji, maeneo ya kilimo na maeneo ya ardhi yaliyo wazi kwa matumizi ya jamii. Serikali itaendelea na zoezi la utambuzi na usajili wa ardhi na kuanza mpango wa kufukia bahari (reclamation) kwa lengo la kupata ardhi kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

**MIUNDOMBINU YA USAFIRI NA USAFIRISHAJI**

Miundombinu ya usafiri na usafirishaji ikiwemo barabara na viwanja vya ndege ina umuhimu mkubwa katika kuchochea ukuaji wa uchumi, kuimarisha huduma na kuchochea uwekezaji.

Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Serikali itaendeleza ujenzi wa miundombinu ya usafiri kwa kujenga barabara ya Tunguu-Makunduchi (km 48), Fumba – Kisauni (km 12), Mkoani – Chake (km 43.5) na barabara za Utalii Nungwi (km 12) pamoja na kuweka taa za barabarani katika maeneo yote hayo ikiwemo barabara za ndani.

Serikali imedhamiria kuweka taa za kuongozea gari katika makutano 10 ya barabara yakiwemo Mpendae, Mkunazini, Malindi, BOT Kinazini, Mikunguni kwa Pweza, Mtoni na Saateni kwa Unguja na Machomane, Chanjaani (njia ya uwanja wa ndege) na Melitano kwa Pemba.

Pia, itaendeleza ujenzi wa barabara za mjini km 100.9, vijijini km 275 na barabra mpya za mjini km 333.7. Pia, itakamilisha ujenzi wa daraja na barabara ya Unguja Ukuu - Uzi na kujenga daraja litakalopita baharini la kuunganisha kijiji cha Chwaka na Charawe ili kuunganisha barabra baina ya Mkoa wa Kusini (U) na Mkoa wa Kaskazini (U).

Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, serikali ina lengo la kuongeza idadi ya abiria wanaotumia viwanja vya ndege kutoka 2,140,986 kwa mwaka hadi kufikia abiria 2,824,011 ili kuongeza kipato na ajira.

Ili kufikia azma hiyo, uimarishaji wa miundombinu ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume kwa ujenzi wa majengo na ukarabati wa baadhi ya majengo ya zamani, kujenga vituo viwili vya mafuta ya ndege na karakana ya kufanyia matengenezo ya ndege na kuongeza eneo la maegesho ya ndege kwa mita za mraba 106,000.

Aidha, kutaendelezwa ujenzi wa njia ya kurukia ndege katika kiwanja cha ndege cha Pemba na kujenga jengo jipya la abiria.

**MAENDELEO YA MIPANGO MIJI, NYUMBA NA MAKAZI**

Serikali iliahidi kuendelea kusimamia maendeleo ya miji na kuwapatia wananchi nyumba bora za makaazi, katika kipindi hiki tutaendelea kwa kukamilisha ujenzi wa nyumba mpya za makaazi 4,715 katika maeneo ya Chumbuni, Nyamanzi na Kisakasaka kwa Unguja na Mfikiwa Pemba kwa ajili ya wananchi wa kipato cha chini, ambapo kutaandaliwa sera maalum ya makazi bora yenye kufuata mpangilio na kupendezesha miji yetu, kutaandaliwa mpango bora wa matumizi ya ardhi na kuongeza asilimia ya watu wanaoishi katika makaazi yaliyofuata mipango miji kutoka asilimia 18 mwaka 2025 hadi asilimia 40.

**UWEZESHAJI WA WANANCHI KIUCHUMI**

Serikali inazingatia umuhimu mkubwa wa haja ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi kutokana na faida zake kwa maendeleo yao binafsi na nchi yetu kwa jumla. Katika kuendeleza dhamira hiyo, Serikali kupitia Mamlaka ya Uwezeshaji wananchi kiuchumi itatoa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 100 kwa wananchi pamoja na kuwapatia mafunzo ya usimamizi wa fedha kwa wajasiriamali wazalishaji na wafanyabiashara.

Pia, itawapatia mafunzo ya uzalishaji na kuwaunganisha na masoko. Aidha, mikopo kutoka Serikali za Mitaa itatolewa kwa mgawanyo wa asilimia 40 kwa vijana, asilimia 40 kwa wanawake na asilimia 20 kwa watu wenye ulemavu.

Serikali itatoa mikopo kwa wajasiriamali wakubwa ili kuwawezesha kuwaajiri vijana. Pia itaendelea kujenga masoko mapya kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo na wajasiriamali katika maeneo mbali mbali yakiwemo Kibanda maiti, Kwa haji tumbo, Fuoni, Kinyasini (U) na kukamilisha ujenzi wa soko la Mombasa ili kuwawezesha kufanya shughuli zao katika mazingira bora.

**FURSA ZA AJIRA KWA VIJANA**

Uwepo wa mahitaji makubwa ya ajira kwa wananchi hususan vijana hapa nchini yamepewa kipaumbele na Serikali ya Awamu ya Nane ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Katika kukabiliana na changamoto ya ajira pamoja na mambo mengine, Serikali katika kipindi hiki itaendeleza program za kukuza ujuzi kwa vijana ambao watapewa mafunzo kazini na taaluma kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kujiajiri na kuajirika katika sekta za umma na binafsi, kuendeleza utaratibu wa kulinda fursa za ajira kwa vijana wazawa kupitia sera na sheria, kuandaa program maalum za kuwavutia wawekezaji wa sekta binafsi kwa lengo la kuajiri vijana na kutoa mafunzo mahsusi ikiwemo ujuzi wa fani adimu ambazo vijana wanashindwa kupata fursa za ajira kwa kukosa ujuzi unaohitajika.

Serikali itaandaa mpango maalum wa kuwaibua vijana wajasiriamali mabingwa na kuwawezesha kukuza miradi yao ili waweze kuajiri vijana wengine na kutoa mafunzo na usimamizi kwa wajasiriamali wapya.

Lengo la jumla la Serikali katika kipindi cha miaka mitano ni kuzalisha ajira mpya 350,000 kwa



# YAJAYO NI NEEMA ZAIDI, UONGOZI UNAOACHA ALAMA VIPAUMBELE MIAKA MITANO IJAYO YA DKT. MWINYI MADARAKANI



wananchi wa Zanzibar hasa vijana katika sekta rasmi na zisizo rasmi.

**MAENDELEO YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

Serikali inatilia mkazo maendeleo ya Sayansi na Teknolijia ili kuongeza kasi ya maendeleo kiuchumi na huduma za jamii. Serikali itaimarisha mazingira ya uchumi wa kidijitali na kuongeza upatikanaji wa teknolojia mpya.

Serikali itaimarisha uwekezaji katika miundombinu ya TEHAMA na kujenga vituo vya teknolojia vinavyokidhi viwango vya kimataifa, pamoja na kuanzisha majukwaa ya mtandaoni na mifumo ya biashara inayosaidia masoko ya ndani, ya kanda na kimataifa.

Pia, Serikali itaimarisha uchumi wa kidijitali kwa kuzingatia thamani yake kubwa kama nyenzo muhimu kwa ustawi wa sekta nyengine, utoaji wa huduma na uendeshaji wa shughuli za Serikali.

Shughuli za utafiti na ubunifu zitapewa msukumo ili kuchochea ufanisi katika utekelezaji wa mipango yetu ya maendeleo.

**HUDUMA ZA JAMII**

Kuimarisha huduma za jamii ikiwemo afya, elimu na maji safi na salama ni miongoni mwa vipaumbele vya Serikali kwa kuzingatia umuhimu wa huduma hizo kwa ustawi wa wanajamii.

Katika sekta ya afya Serikali ina lengo la kuendeleza mafanikio yaliyopatikana kwa kujenga hospitali 4 mpya za Mikoa ya Kusini (U), Kaskazini (U) Kusini (P) na Kaskazini (P), kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi, kuendelea na ukarabati wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, kujenga hospitali ya rufaa na kufundishia ya kisasa Binguni, kuendeleza ujenzi wa hospitali ya wagonjwa wa akili Pemba na kuimarisha miundombinu na upatikanaji wa huduma bora za afya ya msingi ikiwemo ujenzi na ukarabati wa vituo vya afya.

Kwa kutambua umuhimu wa sekta ya elimu katika kuandaa nguvukazi na kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii, Serikali itaendelea kuimarisha sekta hiyo katika miaka mitano ijayo.

Serikali itaendelea kuipa kipaumbele sekta ya elimu kwa kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya elimu, kuzipatia skuli vifaa vya kujifunza na kufundishia, vifaa vya maabara za masomo ya Sayansi na Teknolojia, kutoa mafunzo ya ualimu na kuhakikisha kiwango cha ufaulu wa wanafunzi katika mitihani ya taifa kinazidi kuongezeka.

SMZ itaendelea kujenga madarasa mapya 2,000 katika skuli 29 za ghorofa za msingi na sekondari. Skuli 3 za sekondari za wanawake zitajengwa kwa kila Mkoa kuimarisha upatikanaji wa fursa ya elimu ya sekondari kwa watoto wa kike, kuimarisha mafunzo ya elimu ya amali na kujenga dakhalia katika kila Wilaya kwa mujibu wa mahitaji.

Pia Serikali itaimarisha utoaji na usimamizi wa mikopo ya wanafunzi na kuongeza idadi ya wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu kutoka 8,870 mwaka 2024 hadi kufikia 20,000. Kuimarisha mafunzo ya ualimu kwa kujenga Chuo cha kisasa cha mafunzo ya ualimu, tutaajiri walimu wapya 7,691 na kuimarisha maslahi ya walimu.

Kuhusu huduma za maji safi na salama, Serikali itaendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma hiyo kwa kuendeleza jitihada zilizoanza za ujenzi wa miundombinu ya maji safi na salama katika maeneo yote ya nchi yetu. Serikali itaongeza juhudi kwa kuimarisha miundombinu ya uzalishaji, usambazaji na kuunganisha huduma za maji safi na salama wananchi.

Serikali katika kipindi chake cha pili cha miaka mitano ya uongozi wake, itaendelea kuweka mazingatio makubwa katika kuhakikisha ustawi na maendeleo ya makundi maalum yakijumuisha watu wenye ulemavu, wanawake, watoto na wazee.

Serikali itashajiisha upatikanaji wa ajira zenye staha kwa watu wenye ulemavu, itahakikisha wanashirikishwa katika shughuli mbali mbali za maendeleo pamoja na kuzilinda na kuziimarisha haki zao.

Itaongeza uwiano wa watu wenye ulemavu katika kupata huduma na kuendelea kutoa ruzuku kwa jumuiya za watu wenye ulemavu ili kuwapa fursa ya kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi.

Kwa upande wa wanawake, Serikali inatambua umuhimu wa kuliwezesha kundi hili kwa kukuza usawa na haki katika jamii. Serikali itaimarisha mifumo ya uwezeshaji wa wanawake kiuchumi, kuimarisha jitihada za kupambana na vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia, kuanzisha na kuimarisha mitandao ya wanawake ili kusaidia kubadilishana maarifa na fursa za maendeleo pamoja na kuendelea kuimarisha ushiriki wa wanawake katika nafasi za maamuzi katika sekta za umma na binafsi.

Mazingatio pia yatawekwa kwa kuwasaidia wajane waweze kujikimu. Kwa kuzingatia kuwa watoto ndio Taifa la kesho, Serikali itahakikisha wanalindwa dhidi ya changamoto mbali mbali ikiwemo udhalilishaji na kukosa malezi bora.

Serikali imenuia kuimarisha mifumo ya hifadhi ya mtoto na kutoa ulinzi ili wawe na mustakabali mwema. Kuhamasisha wazazi kuwalea watoto kwa misingi bora na maadili ili wawe raia wema na kuwaepusha na mazingira hatarishi pamoja na kudhibiti ajira na ndoa za utotoni.

Kuhusu wazee, Serikali inatambua kuwa wao ni hazina kubwa ya hekima, uzoefu, urithi wa mila, desturi na maadili yetu. Serikali itaendelea kuhakikisha hifadhi ya wazee wetu na kuwatunza wakiwemo wanaoishi katika nyumba za wazee Sebleni, Welezo na Limbani.

Wazee wote waliofikia umri wa miaka 70 wataendelea kupatiwa Pencheni jamii. Ahadi ya SMZ na Rais Dkt. Mwinyi ni kuongeza kiwango wanachopata

# YAJAYO NI NEEMA ZAIDI, UONGOZI UNAOACHA ALAMA VIPAUMBELE MIAKA MITANO IJAYO YA DKT. MWINYI MADARAKANI

sasa kwa kadiri hali ya uchumi itakavyoruhusu.

Katika kuimarisha hifadhi ya jamii, Serikali itaimarisha mifumo ya huduma za jamii ili iwafikie wananchi wengi zaidi. Mafao kwa wastaafu yataendelea kulipwa kwa wakati, tutaendeleza huduma za Bima ya Afya kwa wote na kusaidia kaya maskini kwa kuongeza idadi ya wananchi wanaonufaika na fedha za TASAF na fursa za kujiongezea kipato.

**UTUMISHI WA UMMA**

Kwa upande wa watumishi wa umma, Serikali itaendelea kuimarisha mazingira yao ya kufanyia kazi kwa kuwapatia mafunzo, vifaa vya kufanyiakazi na kuongeza maslahi yao ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao ya kuwahudumia wananchi kwa ufanisi zaidi.

Katika kipindi hiki cha miaka mitano ijayo, Serikali ya Awamu ya nane, imenuia kuimarisha uzalendo, nidhamu na uwajibikaji katika Utumishi wa Umma kwa kuweka mifumo madhubuti ya usimamizi wa tabia, uadilifu na utendaji.

Ofisi ya Usalama wa Shughuli za Serikali (GSO) itakua chombo kikuu cha uratibu na ufuatiliaji wa nidhamu Serikalini, ikihakikisha kuwa uwajibikaji na uadilifu vinakua utamaduni wa kudumu katika utumishi wa Umma.

Serikali itaendeleza jitihada za kukabiliana na vitendo vyote vinavyoathiri utekelezaji wa misingi ya utawala bora ikiwemo Rushwa, Uhujumu wa Uchumi na ukiukaji wa maadili ya utumishi. Serikali itazidi kuijengea uwezo wa vifaa vya kisasa, mafunzo na watumishi Mamlaka ya kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA) ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Jitihada za makusudi zitafanywa kuiwezesha Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuongeza uwezo wa Ofisi kutumia mifumo na kwenda sambamba na mabadiliko ya tasnia ya ukaguzi wa matumizi ya fedha za umma.

Kuhakikisha viongozi wote katika utumishi wa umma wanazingatia sheria na maadili ya utumishi katika utekelezaji wa majukumu yao kwa mujibu wa sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Kufanikiwa kwa dhamira ya Serikali ya kuwa na Utumishi wa umma bora, wenye nidhamu na uwajibikaji kuna tegemea mchango wa kila mmoja wetu.




**HABARI NA MAWASILIANO**

Serikali itaendelea kuimarisha ubora na upatikanaji wa habari kupitia redio, televisheni, magazeti na mitandao ya kijamii katika maeneo yote ya Zanzibar.

Kuendelea kuwekeza na kuimarisha miundombinu ya Shirika ka Utangazaji la Zanzibar (ZBC) ili kuimarisha huduma za utangazaji na kukamilisha miundombinu ya kiwanda cha uchapishaji wa magazeti ya Serikali ili kuongeza ufanisi.

Kwa upande wa sekta ya mawasiliano, Serikali itaanzisha mji wa kidijitali (smart city) katika maeneo ya uwekezaji Fumba, kuboresha mawasiliano ya simu katika visiwa vidogo vidogo, kuimarisha mfumo wa Serikali mtandao katika utendaji wa Serikali ili kuongeza ufanisi pamoja na kuweka majina ya mitaa na barabara kwenye mfumo wa anwani za makaazi kwa

wananchi ili wazitumie na kuimarisha huduma za mawasiliano nchini.

**UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**

Serikali inatambua na kuthamini umuhimu wa sekta ya utamaduni, sanaa na michezo katika kuimarisha maendeleo ya nchi yetu. Sanaa na utamaduni zitaendelezwa kwa kuimarisha juhudi za kuendeleza urithi wa Kiswahili, historia, sanaa na utamaduni wa Mzanzibar ili kuvutia watafiti, wanafunzi na watalii wa utamaduni duniani kote.

Serikali itajenga vituo viwili (2) vya kuendeleza sanaa na urithi wa utamaduni katika maeneo ya kimkakati Unguja na Pemba ambapo wageni watajifunza historia, mapishi na mavazi ya Kizanzibari pamoja na kuandaa matamasha ya kimataifa ya utamaduni ikiwemo ya chakula na ya mavazi ya Mzanzibari ili kuvutia watalii na kuutangaza utamaduni wetu.

Kwa upande wa michezo, Serikali itaimarisha sekta hii kwa kuendelea kujenga miundombinu bora ya michezo. Serikali itajenga na kukarabati miundombinu ya michezo na burdani ikiwemo viwanja na vituo vya michezo na utamaduni vinavyokidhi hadhi ya kitaifa na kimataifa kila Wilaya.

Serikali itaanzisha Skuli mbili (2) za akademia za michezo kwa lengo la kukuza na kuendeleza vipaji vya michezo. SMZ itafanya juhudi za kuongoza ushiriki wa wanamichezo wa Zanzibar katika mashindano ya kikanda na kimataifa na kukamilisha maandalizi yetu ya kuwa wenyeji wa mashindano ya AFCON, 2025 kwa kujenga na kuimarisha miundombinu ya michezo na kuboresha miundombinu wezeshi ya malazi usafiri na huduma za tiba

**KUDUMISHA MAPINDUZI, KUENDELEZA MUUNGANO**

Mapinduzi matukufu ya Zanzibar na Muungano wa Tanzania ni tunu muhimu kwa maendeleo na ustawi wa taifa letu. Serikali itaendelea kuyatafsiri malengo ya Mapinduzi kwa vitendo na kuhakikisha yanadumishwa kwa dhamira ile ile ya waasisi wetu kuwa ni kupata uhuru na maendeleo ya Zanzibar.

Serikali ya Zanzibar itaendelea kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuhakikisha wanaendeleza Muungano uliopo kwa kuuimarisha ili uzidi kuleta manufaa kwa wananchi wa pande zote mbili na kuwa msingi muhimu wa amani, umoja na maendeleo yetu.

# MAFANIKIO YA MAPINDUZI KWA MAENDELEO YA ZANZIBAR



SHEIKH ABEID KARUME



ABOUD JUMBE MWINYI



ALI HASSAN MWINYI



IDRISA ABDULWAKIL

MAADHIMISHO ya miaka 62 ya Mapinduzi ya Zanzibar yaliyotokea Januari 12, 1964 ambayo yaliongozwa na Sheikh Abeid Amani Karume pamoja na Kamati ya watu 14 ya wanamapinduzi na kumuondoa Sultan.

Mafanikio ni mengi yaliyopatikana ndani ya miaka 62 ya Mapinduzi ikiwemo kusaidia kupatikana kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar iliyoongozwa na Waafrika na kuleta maendeleo makubwa na kuondosha pengo lililokuwepo la wasionacho.

Miaka 62 ya Mapinduzi ya Zanzibar, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imefanikiwa kuongozwa na viongozi kwa awamu nane ambao wameleta mageuzi makubwa ya kimaendeleo na kusimamia misingi ya mapinduzi.

**KARUME**

Sheikh Karume alikuwa Rais wa Serikali ya Zanzibar na Baraza la Mapinduzi kuanzia Januari 12, 1964 hadi Aprili 7, 1972 ambapo alichukua hatua madhubuti katika kuwaletea maendeleo wananchi ikiwemo kuimarisha huduma za kijamii ndani ya sekta ya afya, elimu, usafiri, na makazi ambapo alitoa bila ya ubaguzi wa rangi, dini au kabila.

Hayati Karume alitangaza kutolewa kwa elimu yenye misingi ya ukabila na kwa malipo ambapo tangazo hilo ilileta fursa kwa watoto wote kufaidika na huduma hiyo na kwamba hatua hiyo ilifuatia maamuzi ya kutaifisha shule 11 binafsi na kupiga marufuku ajira za watoto.

Pia, serikali ilijenga shule vijijini ambako hakukuwa na huduma hiyo ya elimu wakati wa ukoloni ambapo watoto wengi wakiafrika walipata elimu kwa chini ya asilimia 10 licha

ya kuwa walikuwa zaidi ya asilimia 80 ya watoto wote visiwani humo.

Serikali iliimarisha sekta ya elimu ambapo katika Usultan kulikuwa na shule tatu za sekondari ambazo zilikuwa na wanafunzi 743, ikilinganishwa na kabla ya mapinduzi,

serikali ya SMZ iliongeza shule za sekondari ambapo kulikuwa na wanafunzi 10,161 huku kwa upande wa shule za msingi mwaka 1963 kulikuwa na shule 62 na zenye wanafunzi 19,106. Shule hizo ziliongezwa na kufikia 100 na zikiwa na wanafunzi 45,356.

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilianzishwa mpango wa ugawaji ardhi kwa wananchi wote chini ya utaratibu wa heka tatu ambapo sera hiyo ili wawezesha wananchi wengi kumiliki ardhi, mashamba ambapo asilimia kubwa ya mashamba hayo ni ya mikarafuu na minazi ambayo ilikuwa mali ya wachache yaligawiwa kwa wananchi maeneo mbalimbali ikiwemo ya Dole.

Viwanda vyote ambavyo viliendeshwa na watu binafsi, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilitaifisha ikiwemo viwanda vya uzalishaji mafuta ya nazi, mazulia na sabuni ambapo zaidi ya asilimia 80 ya pato yalikuwa yanatokana na sekta hiyo ya viwanda iliongezeka kutoka sh.milioni 22 hadi sh.milioni 49.

Hali hiyo ilisaidia kuongeza ajira kwa wananchi,kukuza uchumi na kupunguza kiasi kikubwa cha uagizaji wa bidhaa za nje na kupunguza matumizi ya fedha za kigeni.

Mei 4, 1970, Rais Karume aliweka jiwe la msingi katika ujenzi wa nyumba za ghorofa 132 eneo la Michenzani na kwamba ujenzi wa ghorofa moja iligharimu sh.milioni 4,752,000 na serikali yake ilikusudia kujenga maghorofa 7000 katika mji wa Zanzibar na kutoa nafasi za makazi kwa wananchi 30,000.

**ABOUD JUMBE**

Kuanzia 1972 hadi 1984, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliongozwa na Aboud Jumbe Mwinyi ambapo alileta mabadiliko makubwa ya kisiasa, kimaendeleo licha ya kukumbana na matatizo kadhaa ya kiuchumi, ikiwemo kushuka kwa bei ya karafuu katika soko la dunia, kupanda kwa bei za bidhaa zilizoagizwa nje na kuanguka kwa thamani ya sarafu ya Tanzania.

Wakati huo, hali ya kiuchumi visiwani humo iliathiriwa sana kupanda kwa bei bei za bidhaa za kilimo ambapo katika mwaka 1979 gharama za uagizaji wa mafuta ya petroli Zanzibar ilipanda kutoka sh.1.77 kwa lita hadi sh. 3.17 kwa lita mwaka 1980 pia bei ya uagizaji mchele ilipanda kutoka sh. 2, 6888 kwa tani mwaka 1979 hadi sh.3,895 kwa tani kwa mwaka 1980.

Kuwepo kwa matatizo hayo, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilifanya juhudi za kuongeza pato la taifa hadi sh. milioni 15 kwa mwaka 1980 ikiwa sawa na asilimia 49 kutokana na

kutegemea zaidi viwanda vya ndani kwa ajili ya bidhaa za matumizi ya nyumbani ikiwemo sabuni, mafuta ya kupikia.

**ALI HASSAN MWINYI**

Kuanzia Januria 31, 1984 hadi Oktoba 17, 1985, Hayati Rais Ali Hassan Mwinyi aliiongoza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na uongozi wake ulileta maendeleo makubwa ikiwemo kuweka ukarasa mpya wa historia ya Zanzibar kibiashara.

Hali hiyo ilitokana na kuwaruhusu wafanyabiashara kuingiza bidhaa mbalimbali. Uamuzi huo ulisaidia wananchi kupata bidhaa mbalimbali na kusaidia kukua kwa sekta ya biashara ambapo katika kipindi cha Juni, 1984 hadi Machi, 1985 bidhaa zenye thamani ya sh.milioni 134 zilingizwa Zanzibar.

Pia, bidhaa zenye thamani ya sh.milioni 2 zilisafirishwa na kwamba hayo yalikuwa mabadiliko makubwa ya kibiashara katika kipindi kifupi ch utawala wake ambao ulikuwa ukitekeleza sera ya biashara huria.

**IDRISA ABDULWAKIL**

Idrisa Abdulwakil alikuwa Rais wa Zanzibar kuanzia Oktoba 17, 1985 hadi Oktoba 25, 1990 ambapo alianzisha

# MAFANIKIO YA MAPINDUZI KWA MAENDELEO YA ZANZIBAR

sera ya Mtakula iliolenga kuwahamasisha wananchi wa Zanzibar kuzalisha zaidi mazao ya chakula na ya kibiashara.

Lengo la kufanya hayo ni kuongeza kiwango cha mazao ya biashara na ya chakula na kuongeza usafirishaji wa nje wa bidhaa za kilimo na kupunguza mzigo kwa serikali kuagiza chakula kutoka nje.

Alisaidia ongezeko la ajira ya wafanyakazi wa serikali ambapo zaidi ya wafanyakazi 26,500 waliajiriwa huku nafasi za watendaji wa serikali ziliongezeka kwa asilimia 10 kutoka nafasi 20,000 hadi 22,000, kulikuwepo na ongezeko la asilimia 16 la wafanyakazi kutoka wafanyakazi 17,700 hadi 20,500.



DKT. SALMIN AMOUR



AMANI ABEID KARUME



DKT. ALI MOHAMMED SHEIN

**DK. SALMIN AMOUR**

Kuanzia Oktoba 25, 1990 hadi Novemba 8, 2020, Dk. Salmin Amour aliiongoza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambapo alifufua uchumi wa Zanzibar kwa kuendeleza yale yalioanzishwa na watangulizi wake ikiwemo kuweka mkazo wa kukuza biashara huru na kukaribisha wawekezaji kutoka nje na ndani.

Pia, alibinafsisha mashirika ya sekta za umma ambayo yalikuwa yakiendeshwa kwa hasara na kutegemea ruzuku kutoka serikalini, ambapo mabadiliko yote hayo ya kiuchumi yalilenga kuondokana na uchumi tegemezi wa zao moja la karafuu ambalo bei yake katika soko la dunia iliteremka.

Alianzisha maeneo huru ya kiuchumi ikiwemo Fumba, Micheweni na Amani eneo la viwanda vidogo vidogo ambapo maeneo hayo yalitoa fursa kwa wawekezaji binafsi wa nje na ndani kuanzisha miradi ya viwanda na sekta za uazalishaji kwa kushirikiana na sekta binafsi.

Pia, kwa upande wa kisiasa mfumo wa vyama vingi uliofutwa visiwani humo tokea mwaka 1964 baada ya mapinduzi kufaulu ambapo lengo ni kurejeshwa kwa uhuru zaidi kwa wananchi kutumia demokrasia kuiendesha nchi yao.

Biashara iliongezeka ikiwemo uagizaji wa bidhaa kutoka nje uliongezeka na kusaidia uchumi wa Zanzibar kukua kwa wastani wa asilimia 4.3 huku pato la mtu binafsi nalo liliongezeka kwa asilimia 62 kutoka sh.90,645 kwa mwaka 1995 hadi sh.147,433 kwa mwaka 1998.

**AMANI ABEID KARUME**

Novemba 8, 2000 hadi Novemba 3, 2010, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliongozwa na Aman Abeid Amani Karume ambaye naye aliweza kuleta maendeleo makubwa ikiwemo kusaidia kuongezeka kwa pato la mtu mmoja kufikia dola za

kimarekani 557 kutoka dola za kimarekani 260 katika mwaka 2000.

Mafanikio hayo yalisaidia kukuza uchumi wa Zanzibar ambapo ulikuwa kwa asilimia 6.7 ikilinganishwa na asilimia 4.3 iliyokuwepo awali huku pato la taifa nalo likiongezeka na kufikia thamani ya sh.milioni 878,400.

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ulianzisha miradi mikubwa ya sekta ya nishati ambapo mradi wa upelekaji umeme Pemba kutoka Tanga ulifanikiwa kumalizika huku ujenzi wa miundombinu ya barabara ya kurukia na kutulia ndege katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Zanzibar ulikamilika.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar alisaidia uwezeshaji wananchi kiuchumi ikiwemo kutoa sh.bilioni 1.2 kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kiuchumi, ambapo hadi kufikia

Machi,mwaka 2010 zaidi ya sh.1,283,640,000zilitolewakwa vikundi vya Kuweka na Kukopa (SACCOS) na watu binafsi katika maeneo ya Unguja na Pemba.

Serikali ya Awamu ya Sita ilijikita zaidi katika kuwahamasisha wananchi katika uzalishaji wa mazao ya kibiashara na ya vyakula ambapo uzalishaji wa mpunga uliongezeka kutoka tani 20,569 mwaka 2008 hadi tani 26,962 mwaka, 2009 huku zao la muhogo likiongezeka kutoka tani 149,192 mwaka 2008 hadi kufikia tani 155,546 mwaka 2009,kwa upande wa viazi pia uzalishaji ulipanda kutoka tani 3,413 mwaka 2008 hadi tani 11,372 mwaka 2009.

Serikali ilifanikiwa kutekeleza miradi ya sekta ya maji ikiwemo ujenzi wa miradi mbalimbali ikiwemo visima vitano, ujenzi wa matanki mawili, ujenzi wa barabara za kimkakati ikiwemo ya Mazizini - Fumba, PwaniMchangani - Mshelishelini na Mkoani - Makombeni, Amani-Dunga, Wete-Konde na Mtambile-Kengeja.

**DKT. ALI MOHAMMED SHEIN**

Rais mstaafu Dkt. Ali Mohammed Shein aliingia madarakani kuanzia Novemba 3, 2010 hadi Novemba 3, 2020 alileta maendeleo makubwa kwa wananchi wa Zanzibar ikiwemo kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ikiwemo kuimarisha hali ya uchumi kwa kuongeza pato la taifa na ukuaji wa uchumi.

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar alidhibiti mfumuko wa bei kwa kufuatilia kwa undani mwenendo wa bidhaa na huduma, alisaidia kupanda kwa makusanyo ya mapato ya ndani ya serikali alishusha misamaha isiokuwa na tija ya kodi.

Lengo kubwa ni kuimairisha makusanyo ya mapato na kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka kwa wahisani kwa asilimia 12.2 ya bajeti hadi asilimia 11.1 na kusaidia kuleta kasi ya ukuaji wa kiuchumi kwa wananchi.

Alifanikiwa kuondoa kuondoa michango katika shule, alinunua meli ya MV Mapinduzi II, aliboreshea maslahi ya watumishi wa umma ikiwemo kuongeza nyongeza ya mishahara ya watumishi wa umma kwa asilimia 100 wa kima cha chini kutoka sh.150,000 hadi sh.300,000 kwa kuzingatia elimu na miundo ya utumishi (Scheme of Service).

Aliwezesha utoaji wa pensheni kwa wazee, alikamilisha ujenzi wa barabara ya7

Ole-Kengeja yenye urefu wa kilomita 35, Mkanyageni-Kangani ya kilomita 6.5, Finya- Ficha yenye kilomita 8.8 na Mgagadu-Kiwani ya kilomita 7.6 kwa upande wa Pemba.

Aliwezesha ujenzi wa shule za elimu ya awali, kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi, na kusaidia ujenzi wa miundombinu mbalimbali ambayo ilikuwa chachu ya mafanikio kwa Wananchi wa Zanzibar.



# MAFANIKIO YA MASHIRIKA YA UMMA KWA MAENDELEO YA ZANZIBAR



***Dkt. Juma Malik Akil***
***WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO***



***Waheed Muhammed Ibrahim Sanya,***
***MSAJILI WA HAZINA ZANZIBAR***

# IDARA YA MITAJI YA UMMA YAPATIWA MAFUNZO KUHUSU USIMAMIZI WA TAASISI ZA UWEKEZAJI ZA UMMA

*Idara ya Mitaji ya Umma na Uwekezaji Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar wakipatiwa mafunzo juu uanzishwaji wa Kampuni Tanzu katika Mashirika ya Umma mafunzo hayo yametolewa na Wakufunzi kutoka Ofisi ya Msajili wa Hazina Tanzania Bara.*



Watumishi wa Idara ya Mitaji ya Umma na Uwekezaji kutoka Ofisi ya Msajili wa Hazina – Zanzibar wamenufaika na mafunzo maalum ya kujenga uwezo kuhusu usimamizi wa Taasisi za Uwekezaji za Umma, yaliyofanyika katika Ofisi ya Msajili wa Hazina Tanzania Bara kuanzia tarehe 01 hadi 05 Disemba, 2025.

Mafunzo hayo yalilenga kuwawezesha watumishi hao kupata uelewa wa kina juu ya mbinu bora za kusimamia uwekezaji wa umma kwa kuzingatia ufanisi wa kiutendaji, utawala bora, uendelevu wa biashara na maslahi mapana ya Taifa. Ziara hiyo ni sehemu ya juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuimarisha usimamizi wa mali na mitaji ya umma ili kuongeza mchango wake katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo, mmoja wa wawezeshaji kutoka Ofisi ya Msajili wa Hazina Tanzania Bara alieleza kuwa usimamizi thabiti wa Taasisi za Uwekezaji za Umma unahitaji mifumo madhubuti ya kifedha, mipango endelevu ya biashara, pamoja na ufuatiliaji wa karibu wa utendaji wa mashirika hayo.

Katika mafunzo hayo, washiriki walijifunza masuala mbalimbali ikiwemo Sera ya Usimamizi wa Uendelevu wa Biashara **(Business Continuity Management Policy – BCM),** Mpango wa Uendelevu wa Biashara **(Business Continuity Plan – BCP),** taratibu za uanzishaji na usimamizi wa kampuni tanzu (subsidiary companies), pamoja na mbinu za kubadilisha madeni ya mashirika ya umma kuwa mtaji wa Serikali **(debt-to-equity conversion).**

Aidha, mafunzo yalijikita katika mbinu za kusimamia mashirika ya umma ili kuongeza tija na uendelevu wa kiutendaji kwa kuzingatia vipengele muhimu vya utendaji wa kifedha, ufanisi wa uendeshaji, utawala bora, usimamizi wa vihatarishi, rasilimali watu na masuala ya mazingira, kijamii na uendelevu.

Washiriki walielezwa kuwa Ofisi ya Msajili wa Hazina ina jukumu la kuhakikisha Taasisi za Uwekezaji za Umma zinapunguza utegemezi wa kifedha kutoka Serikali Kuu na badala yake kuchangia mapato ya Serikali kupitia gawio na mchango mwingine wa kiuchumi. Hivyo, uimarishaji wa uwezo wa watumishi ni hatua muhimu katika kufanikisha azma hiyo.

Kwa upande wao, watumishi wa Idara ya Mitaji ya Umma na Uwekezaji Zanzibar walieleza kuwa mafunzo hayo yamewapatia maarifa mapya yatakayosaidia kuboresha usimamizi wa taasisi zinazomilikiwa au kushirikishwa na Serikali, pamoja na kuimarisha uwajibikaji na ufanisi wa matumizi ya rasilimali za umma.

Kupitia mafunzo hayo, Ofisi ya Msajili wa Hazina – Zanzibar inatarajia kuimarisha ushirikiano na Ofisi ya Msajili wa Hazina Tanzania Bara, kuandaa miongozo mbalimbali ya kiusimamizi, pamoja na kuweka mifumo bora ya ufuatiliaji wa utendaji wa Taasisi za Uwekezaji za Umma.

Hatua hiyo ni sehemu ya mkakati wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wa kuimarisha utawala bora, kuongeza mapato yasiyo ya kodi na kuhakikisha uwekezaji wa umma unaleta matokeo chanya kwa maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla.




*Watendaji kutoka Idara ya Mitaji ya Umma na Uwekezaji Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar wakipatiwa mafunzo katika ziara waliyoifanmya Ofisi ya Msajili wa Hazina Tanzania Bara.*

# WAHASIBU WAKUU WA MASHIRIKA WAFUNDWA NAMNA BORA YA KUANDAA SERA YA GAWIO





*Ndugu Abdulla Salum Abdulla kutoka Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar akitowa Mafunzo juu ya Kuandaa Sera ya Gawio kwa Mashirika ya Umma Zanzibar*

Idara ya Mitaji ya Umma na Uwekezaji, Ofisi ya Msajili wa Hazina – Zanzibar, imeendesha mafunzo ya siku moja kwa Wahasibu Wakuu wa Mashirika ya Umma kuhusu namna bora ya kuandaa Sera za Gawio, kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa mapato na kuongeza mchango wa mashirika hayo katika maendeleo ya Taifa.

Mafunzo hayo yalifanyika tarehe 11 Disemba, 2025 katika Ukumbi wa Mikutano wa ZURA, ambapo **Afisa Mitaji ya Umma, Ndg. Abdulla Salum Abdulla,** aliwasilisha mada juu ya umuhimu wa kufuata muongozo rasmi wa uandaaji wa Sera za Gawio kwa Mashirika ya Umma wakati wa kuandaa sera zao.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo, **Ndg. Abdulla Salum Abdulla** alieleza kuwa Sera ya Gawio ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha Mashirika ya Umma yanachangia mapato ya Serikali kwa uwazi, uwajibikaji na kwa kuzingatia uendelevu wa kifedha wa mashirika husika. Alisisitiza kuwa uandaaji wa sera hizo unapaswa kuzingatia miongozo iliyowekwa ili kufanikisha malengo ya Serikali ya kuongeza mapato yasiyo ya kodi.

Mafunzo hayo yalihudhuriwa na Wahasibu Wakuu kutoka Mashirika mbalimbali ya Umma, ambapo walipata fursa ya kujifunza kwa kina misingi ya kuandaa Sera za Gawio, ikiwemo kuzingatia hali ya kifedha ya shirika, mahitaji ya uwekezaji, uendelevu wa biashara pamoja na matarajio ya Serikali kama mmiliki au mdau mkuu.

Washiriki wa mafunzo hayo walipongeza jitihada za Idara ya Mitaji ya Umma kwa kuandaa mafunzo hayo na kuahidi kuyafanyia kazi mafunzo waliyopewa ili kuhakikisha Mashirika ya Umma yanaandaa na kutekeleza Sera za Gawio zilizo bora, zinazotekelezeka na zenye kuleta tija.

Kupitia uandaaji na utekelezaji wa Sera za Gawio kwa Mashirika ya Umma, Serikali inatarajia kuongeza mapato yasiyo ya kodi, kuimarisha nidhamu ya kifedha katika mashirika, pamoja na kufikia malengo ya kiuchumi na kijamii yaliyowekwa katika mipango ya maendeleo ya Taifa.

Hatua hiyo ni sehemu ya mkakati wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wa kuimarisha usimamizi wa mitaji ya umma na kuhakikisha rasilimali za umma zinatumika kwa ufanisi kwa manufaa ya wananchi na maendeleo endelevu ya nchi.



*Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar wakitowa Mafunzo juu ya Kuandaa Sera ya Gawio kwa Mashirika ya Umma Zanzibar.*



*Wahasibu Wakuu kutoka Mashirika ya Umma wakitowa Mafunzo juu ya Kuandaa Sera ya Gawio za Mashirika ya Umma Zanzibar.*

**Hatua hiyo ni sehemu ya mkakati wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wa kuimarisha usimamizi wa mitaji ya umma na kuhakikisha rasilimali za umma zinatumika kwa ufanisi kwa manufaa ya wananchi na maendeleo endelevu ya nchi.**

# IDARA YA MITAJI YA UMMA NA UWEKEZAJI YATOWA MAFUNZO KWA BENKI YA WATU WA ZANZIBAR (PBZ) JUU YA KUANDAA RIPOTI ZA UTEKELEZAJI ZA MKATABA WA KIUTENDAJI



***Watendajiw a Idara ya Mitaji ya Umma na Uwekezaji wakitoa Mafunzo kwa Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) Juu ya Kuandaa Ripoti za Utekelezaji za Mkataba Wa Kiutendaji***



***Mafunzo juu ya Kuandaa Ripoti za Utekelezaji za Mkataba wa Kiutendaji yametolewa kwa Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) na Wakufunzi kutoka Idara ya Mitaji ya Umma na Uwekezaji***



***Watendaji wa Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) wakifuatilia Mafunzo juu ya Kuandaa Ripoti za Utekelezaji za Mkataba Wa Kiutendaji wakifuatilia yaliyotolewa na Wakufunzi kutoka Idara ya Mitaji ya Umma na Uwekezaji***

Idara ya Mitaji ya Umma na Uwekezaji, Ofisi ya Msajili wa Hazina – Zanzibar, imetoa mafunzo kwa watumishi wa Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) kuhusu uandaaji wa Ripoti za Utekelezaji wa Mikataba ya Kiutendaji, kwa lengo la kuimarisha ubora, usahihi na ufanisi wa taarifa zinazowasilishwa kwa Serikali.

Mafunzo hayo yalifanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Benki ya Watu wa Zanzibar, ambapo washiriki walielezwa kwa kina umuhimu wa kuandaa ripoti za utekelezaji kwa umakini, kwa kuzingatia viashiria vya utendaji vilivyokubaliwa katika Mikataba ya Kiutendaji. Aidha, mafunzo hayo yalilenga kuhakikisha kuwa taarifa zinazowasilishwa zinaakisi kwa usahihi utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya benki pamoja na maendeleo ya kufikia malengo yaliyowekwa.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo, wawezeshaji kutoka Idara ya Mitaji ya Umma na Uwekezaji walieleza kuwa Mikataba ya Kiutendaji ni nyenzo muhimu ya usimamizi inayosaidia Serikali kufuatilia utendaji wa taasisi zake, kupima ufanisi, pamoja na kuchukua hatua stahiki za kiutawala na kimaamuzi. Hivyo, ubora wa ripoti za utekelezaji ni msingi muhimu katika kuhakikisha mikataba hiyo inaleta matokeo yaliyokusudiwa.

Mafunzo hayo yalisisitiza namna bora ya kuandaa ripoti zenye takwimu sahihi, vielelezo vinavyoeleweka na uchambuzi unaoonyesha changamoto, mafanikio na hatua za maboresho. Washiriki walihimizwa kuzingatia ratiba za uwasilishaji wa ripoti ili kuwezesha tathmini ya utendaji kufanyika kwa wakati.

Kwa upande wao, watumishi wa PBZ walipongeza mafunzo hayo na kueleza kuwa yamewasaidia kuongeza uelewa juu ya mahitaji ya Serikali katika uandaaji wa ripoti za utekelezaji wa Mikataba ya Kiutendaji. Waliahidi kuyatumia maarifa waliyopata ili kuboresha utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku na kuhakikisha malengo ya benki yanafikiwa kwa wakati.

Kupitia mafunzo hayo, Serikali inatarajia kuona ongezeko la uwajibikaji, ufanisi wa kiutendaji na ubora wa taarifa zinazowasilishwa na PBZ, hali itakayochangia katika kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi na kuimarisha mchango wa benki katika maendeleo ya kiuchumi ya Zanzibar.

Hatua hii ni sehemu ya mkakati wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wa kuimarisha usimamizi wa taasisi za umma na kuhakikisha Mikataba ya Kiutendaji inatumika ipasavyo kama chombo cha kufanikisha malengo ya maendeleo ya Taifa.

# UKUSANYAJI WA MAPATO YASIYO YA KIKODI WAIMARIKA – OFISI YA MSAJILI WA HAZINA ZANZIBAR



*Msajili Wa Hazina Zanzibar Afanikisha Kuimarika Kwa Makusanyo yasiyo ya Kikodi Kupitia Gawio Zanzibar.*

Ofisi ya Msajili wa Hazina imeripoti kuimarika kwa ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kikodi kupitia makusanyo ya gawio kutoka Taasisi za Umma, hali iliyopelekea mapato hayo kufikia jumla ya shilingi bilioni 13.2 hadi sasa. Mafanikio haya ni matokeo ya ufuatiliaji madhubuti wa utendaji wa taasisi, usimamizi thabiti wa rasilimali za umma na kuimarika kwa uwajibikaji wa mashirika ya serikali.

Katika taarifa rasmi iliyotolewa, Ofisi ya Msajili wa Hazina imeeleza kuwa Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC) limeendelea kufanya vizuri katika ukusanyaji wa mapato kutokana na maboresho ya uendeshaji, kuongezeka kwa shughuli za bandari na usimamizi bora wa mapato. Hatua hizi zimechangia kwa kiasi kikubwa kuongeza mchango wa shirika hilo katika mapato ya serikali.

Aidha, Shirika la Meli Zanzibar (SHIPCO) limeonesha kuimarika kwa kiwango cha utoaji wa gawio kwa Serikali, hatua inayodhihirisha mafanikio ya mageuzi ya kiutendaji na kifedha yaliyotekelezwa ndani ya shirika hilo. Kuimarika kwa SHIPCO kumetajwa kuwa mfano wa kuigwa kwa taasisi nyingine za umma katika kuongeza tija na mchango wake kwa maendeleo ya taifa.

Mapato haya yasiyo ya kikodi yanatarajiwa kuisaidia Serikali katika kutekeleza Bajeti Kuu ya Mwaka wa Fedha 2025/2026, hususan katika kufikia malengo ya vipaumbele vya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Serikali imeeleza kuwa itaendelea kuimarisha mifumo ya usimamizi na ufuatiliaji wa taasisi za umma ili kuongeza uwazi, ufanisi na mchango wa taasisi hizo katika mapato ya taifa.

Ofisi ya Msajili wa Hazina imewataka wakuu wa taasisi za umma kuendelea kusimamia vyema rasilimali walizopewa, kubuni mikakati ya kuongeza mapato na kuhakikisha gawio la serikali linaongezeka kwa wakati, ili kuunga mkono jitihada za Serikali katika kukuza uchumi na ustawi wa wananchi.



*Watendajiw a Idara ya mitaji ya Umma na Uwekezaji wakijadili namna bora ya kuboresha ulipaji wa Gawio kwa Mashirika ya Umma.*

# OFISI YA MSAJILI WA HAZINA YAJA NA MIONGOZO YA MIUNDO, MASLAHI NA TATHMINI YA BODI KWA MASHIRIKA YA UMMA

Ofisi ya Msajili wa Hazina Ipo katika hatua za mwisho za uandaaji wa miongozo muhimu itakayosaidia kuimarisha utawala bora, uwajibikaji na ufanisi katika Mashirika ya Umma Zanzibar. Miongozo hiyo ni pamoja na Mwongozo wa Tathmini ya Utendaji wa Bodi (Board Evaluation), Mwongozo wa Uandaaji wa Mapendekezo ya Miundo ya Taasisi za Uwekezaji wa Umma, pamoja na Mwongozo wa Uwasilishaji wa Mapendekezo ya Mishahara na Maslahi kwa Taasisi za Uwekezaji wa Umma.

Miongozo hii imeandaliwa na wataalamu wa Idara ya Mitaji ya Umma kwa kushirikiana na watendaji kutoka Ofisi ya Msajili wa Hazina Tanzania Bara na Utumishi wa Umma, hatua inayoonesha mshikamano wa kitaasisi na dhamira ya Serikali katika kuhakikisha Mashirika ya Umma yanaendeshwa kwa misingi ya kitaalamu na viwango vinavyokubalika.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Msajili wa Hazina, mwongozo wa tathmini ya bodi unalenga kupima kwa uwazi na haki utendaji wa bodi za mashirika ya umma, ikiwemo kiwango cha utekelezaji wa majukumu yao ya kimkakati, usimamizi wa rasilimali, maamuzi wanayoyafanya na mchango wao katika kufikia malengo ya taasisi. Tathmini hii itawezesha kubaini changamoto, kuimarisha uwajibikaji na kuboresha ufanisi wa bodi husika.



*Kamati ya kuandaa Mwongozo wa Uandaaji wa Mapendekezo ya Miundo ya Taasisi za Uwekezaji wa Umma*

Aidha, mwongozo wa uandaaji wa mapendekezo ya miundo ya taasisi za uwekezaji wa umma umeandaliwa ili kusaidia mashirika kuwa na miundo bora, inayozingatia majukumu halisi ya taasisi, ufanisi wa kiutendaji na matumizi sahihi ya rasilimali watu. Kupitia mwongozo huu, mashirika yataweza kuandaa miundo itakayoongeza tija, kupunguza mwingiliano wa majukumu na kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Kwa upande mwingine, mwongozo wa uwasilishaji wa mapendekezo ya mishahara na maslahi kwa taasisi za uwekezaji wa umma unalenga kuweka utaratibu unaoeleweka na wenye uwiano katika kuboresha maslahi ya watendaji wa mashirika ya umma. Mwongozo huu utasaidia kuhakikisha kuwa mapendekezo ya mishahara na maslahi yanazingatia uwezo wa kifedha wa taasisi, kanuni za utumishi wa umma pamoja na motisha stahiki kwa watendaji ili kuongeza ufanisi kazini.

Kwa ujumla, miongozo hii ni nyenzo muhimu katika utekelezaji wa majukumu ya bodi na watendaji wa mashirika ya umma Zanzibar. Inatarajiwa kuwa itachangia kwa kiasi kikubwa kuboresha utendaji wa mashirika, kuimarisha utawala bora, kuongeza tija na hatimaye kukuza mchango wa Mashirika ya Umma katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya Zanzibar.

Ofisi ya Msajili wa Hazina imeeleza kuwa itaendelea kutoa miongozo na usimamizi wa karibu ili kuhakikisha Mashirika ya Umma yanatekeleza majukumu yao kwa ufanisi, kwa kuzingatia sera, sheria na miongozo iliyowekwa na Serikali.

*Kamati ya kunandaa Mwongozo wa Uwasilishaji wa Mapendekezo ya Mishahara na Maslahi kwa Taasisi za Uwekezaji wa Umma wakiwa katika kikao cha kazi cha kuandaa Muongozo huo.*



# OFISI YA MSAJILI WA HAZINA YAPOKEA MAONI YA WADAU KUHUSU MIONGOZO YA MIUNDO NA MISHAHARA KWA TAASISI ZA UWEKEZAJI WA UMMA.



Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina imeandaa Muongozo wa Uandaaji wa Mapendekezo ya Miundo ya Taasisi za Uwekezaji wa Umma pamoja na Muongozo wa Uwasilishaji wa Mapendekezo ya Mishahara na Maslahi kwa lengo la kuimarisha ufanisi, uwajibikaji na matumizi bora ya rasilimali za umma. Katika hatua ya uaandaaji wa miongozo hiyo, wadau mbalimbali walishirikishwa na kutoa maoni muhimu yaliyolenga kuboresha Miongozo hiyo.

Wadau wamesisitiza kuwa mfumo wa uendeshaji unapaswa kuimarishwa, hasa kwa taasisi zilizopata Daraja A, ili kuweza kuongezwa daraja jingine kwa njia iliyo wazi na yenye uwajibikaji. Pia, wameshauri kuwa Afisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi abadilishwe rasmi na kuwa Mtendaji Mkuu wa Taasisi, huku akipatiwa majukumu mapya ya kuongoza mchakato wa kuandaa na kuwasilisha mapendekezo, kuhakikisha maamuzi si tegemezi kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina peke yake.

Kwa upande wa mchakato wa kisheria, wadau wamesisitiza tofauti kati ya ithibati ya bodi na barua ya kuomba ridhaa iangaliewe wazi ili kuepuka mkanganyiko. Pia, walipendekeza sheria ziandikwe kama zinavyosomwa katika sheria husika, na vifungu vyovyote vilivyokataliwa au kusababisha urasimu vifutwe. Aidha, walipendekeza kuwa mapendekezo ya miundo na maslahi ya taasisi yaonyeshwe wazi wakati yanapowasilishwa, ili kuongeza uwazi kwa wadau na wananchi.

Kwa ujumla, maoni haya yanalenga kuhakikisha kuwa taasisi za uwekezaji wa umma zinafuata miongozo iliyo wazi, yenye uwazi na yenye uwajibikaji, huku zikibaki na tija ya kifedha na usimamizi bora wa rasilimali za umma. Utekelezaji wa mapendekezo haya unatarajiwa kuimarisha utawala bora na kuchangia ukuaji endelevu wa uchumi wa Taifa.

Kwa ujumla, wadau wanaunga mkono miongozo hii kama nyenzo muhimu ya kuleta ufanisi katika usimamizi wa Taasisi za Uwekezaji wa Umma. Utekelezaji wake unatarajiwa kuongeza uwazi, kuimarisha utawala bora na kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa Taifa kupitia uwekezaji wenye tija na uwajibikaji.

***Watendaji kutoka Mashirika ya Umma wakitoa Maoni ya Wadau Kuhusu Miongozo ya Miundo na Mishahara kwa Taasisi za Uwekezaji wa Umma.***





***Watendaji kutoka Mashirika ya Umma wakisikilizo wasilisho juu ya Maoni ya Wadau Kuhusu Miongozo ya Miundo na Mishahara kwa Taasisi za Uwekezaji wa Umma.***

# JICHO LA HAZINA

**TOLEO NAMBA 011**
**DESEMBA, 2025**

## MIAKA 62 YA MAPINDUZI

OFISI YA MSAJILI WA HAZINA ZANZIBAR INAMTAKIA KHERI NA FANAKA RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI, **MHESHIMIWA DKT. HUSSEIN ALI MWINYI** KWA KUTEKELEZA MAONO YA WAASISI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA VITENDO.

MENEJIMENTI, WATUMISHI INAMUAHIDI KUSIMAMA MSTARI WA MBELE KUHAKIKISHA MASHIRIKA YA UMMA YANAENDELEA KUWA NA TIJA KUBWA KWA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR.

***MAPINDUZI DAIMA***

**WATUMISHI NA WAKUU WA MASHIRIKA YA UMMA**



Msajili Wa Hazina Zanzibar https://trosmz.go.tz/ info@trosmz.go.tz

**“UWEPO MASHIRIKA YA UMMA IMARA NI KICHOCHEO CHA MAENDELEO YA UCHUMI”**